SportPesa
TSH 433,401,140
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | *150*87#



RC awatimua watu waliojazana mochwari kufuata miili ya ndugu

UKURASA 4


Huu ndiyo utitiri wa utajiri ndani ya uchumi wa bluu
VIJANA WAIOMBA SERIKALI... Tunataka kuwa sehemu ya mpango huu wa maendeleo
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
Wanawake wauza dagaa DRC waeleza wanakwamishwa wapi

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Agosti 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580678
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ahueni tozo miamala ya simu

**BUNGE** laahidi kufanyia marekebisho, kodi ya majengo kwa LUKU kuanza rasmi... *Endelea ukurasa 2*



Spika Job Ndugai

## WB yaimwagia Tanzania tril. 2.7/- kuboresha elimu, barabara vijijini

UKURASA 2



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia) na Mwakilishi Mkaazi wa Benki ya Dunia nchini, Mara Warwick, wakibadilishana nyaraka baada ya kutiliana saini makubaliano ya mkopo wa miradi mitano yenye thamani ya Sh. trilioni 2.7, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 3

### VYAMA 11 VYA SIASA VYATAKA KURA MAONI KUHUSU KATIBA MPYA

MJADALA wa Katiba mpya umeendelea kuchukua sura mpya baada ya vyama 11 visivyokuwa na wabunge bungeni kuiomba serikali kuufufua mchakato wa Katiba kwa kuitisha kura ya maoni...

UKURASA WA 4

### WAFUASI 19 CHADEMA WAFIKISHWA MAHAKAMANI

WAFUASI 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza...

## Sabaya akiri kumiliki silaha

UKURASA 3



**MICHEZO** **MWALIMU KASHASHA AFARIKI DUNIA** UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Tozo miamala ya simu kurekebishwa

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Bunge liko tayari kufanya marekebisho yatakayohitajika kwenye tozo za miamala ya simu zilizopitishwa wakati wa mkutano wa Bunge uliopita.

Aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua kongamano la walimu wenye ulemavu nchini lililoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

"Tulipitisha suala la tozo ya miamala, kwa kweli ndugu zenu wawakilishi hatujapitisha kitu kile kumkomoa mtu yeyote, tumepitisha kwa nia njema kabisa.

"Labda katika nia njema ile kuna maeneo hatukuangalia vizuri, basi tutajaribu kutizama vizuri huko tunapokwenda kama Rais Samia alivyoelekeza.

"Kwa hiyo, mtaona hili jambo la tozo kwa nini tulilijadili sana sana tukaona twende njia hiyo, kama nilivyosema panapohitaji kupiga pasi kurekebisha tutafanya hivyo, ila tukiondoa tozo tumeacha gizani yale malengo yetu yote tuliyotaka kufanya, tutakwama.

"Ila unaweza rekebisha kidogo, kwa mfano unaweza kumbakisha anayetuma akakatwa lakini anayepokea apokee taslimu au tunaweza rekebisha viwango kidogo kama vimezidi sana, basi tukavirekebisha reke-bisha lakini kwa kweli kimsingi tozo watu wasipotoshe, ni kitu muhimu sana kwa nchi yetu," alisema.

Alibainisha kuwa dhamira ya Bunge kupitisha tozo hizo ni kupata fedha zitakazoelekezwa kusaidia ujenzi wa madarasa ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Spika Ndugai alisema kuwa ndani ya miaka mitano, serikali imepanga kukusanya Sh. trilioni tano ambazo zitatumika katika ujenzi huo wa madarasa pamoja na kusaidia mikopo ya elimu ya juu.

"Bunge litaendelea kujadili suala la tozo kama Rais alivyoelekeza lakini tulifanya hivyo kwa manufaa ya taifa, kwa sababu tunahitaji kuona madarasa ya shule za vijijini yawe kama ya mjini," alisema.

**KURA VITI MAALUM**

Kuhusu upatikanaji wa wabunge wa viti maalum, Spika Ndugai alisema ni vyema uwapo mfumo wa wabunge hao kupatikana kwa kupigiwa kura na wananchi moja kwa moja badala ya sasa ambapo wanachaguliwa kupitia makundi maalum.

"Tukienda nchi za wenzetu tunapata shida, tunaulizwa maswali kuhusu tofauti ya wabunge wa viti maalum na wabunge wengine ikoje, unakuta mtu anatuuliza hivi bungeni kuna viti aina mbili.

"Pale bungeni tuna kundi linawakilisha wenye ulemavu Tanzania, bahati mbaya au nzuri wanatoka kwenye kundi la lile viti maalum CCM kwenye kundi la wanawake.

"Hatujaweza kuwa na mfumo mpaka sasa wa kuwa na wawakilishi wa wenye ulemavu wa moja kwa moja wa kuchaguliwa moja kwa moja na wananchi.

"Kwa hiyo huko mbele kwa sababu nchi inabadilika na mambo yanabadilika, ninafikiri muwe mnafikiri namna gani siku moja tunaweza kuwa na wawakilishi ambao wamechaguliwa na wenye ulemavu wenyewe kwa upana wake wa kura moja kwa moja sio kwa kupitia vyama.



Baadhi ya maofisa operesheni wa Jeshi la Polisi, kutoka mikoa mbalimbali wakiwa kwenye mafunzo ya ulengaji wa shabaha unaoongozwa na Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas katika uwanja wa medani za kivita Mkomanzi, mkoani Tanga jana. **PICHA: JESHI LA POLISI.**

# WB yaimwagia Tanzania tril. 2.7/- kuimarisha elimu, barabara vijijini

**Na Romana Mallya**

SERIKALI na Benki ya Dunia (WB) zimetiliana saini mikataba mitano ya mikopo ya masharti nafuu kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.167 sawa na Sh. trilioni 2.697.

Fedha hizo zinatarajia kutumika katika utekeleza wa miradi mitano Tanzania Bara na Zanzibar.

Miradi hiyo ni ya kuboresha barabara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi (RISE), kuimarisha mazingira ya kujifunzia elimu ya juu (HEET) na kuongeza upatikanaji wa huduma bora za mtandao kwa kuwezesha serikali kwa kuzitoa kidigitali (DTP).

Mingine ni mradi wa kuongeza ufikiwaji wa huduma bora na za uhakika za umeme pamoja na kuongeza uzalishaji mbadala Zanzibar (ZESTA) na mradi wa kuongeza uwezo wa ufikiaji wa hali ya bora za maisha na utoaji huduma katika maeneo nufaika visiwani humo (BIG-Z).

Utiaji saini huo ulifanywa jana jijini Dar es Salaam na Tanzania iliwakilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia Tanzania, Mara Warwick na baadaye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kassim Ali, alitia saini kwa niaba ya Zanzibar.

Waziri Nchemba alisema WB imebaki kuwa mshirika wa kuaminika hata wakati wa matatizo na kwamba serikali inatarajia kuendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya pande zote.

"Mikataba ya mikopo ambayo tumetia saini leo inaongeza thamani ya miradi inayofadhiliwa na benki hii kufikia Dola za Kimarekani milioni 5,502.4, hivi sasa serikali inakamilisha awamu nyingine ya miradi ya kipaumbele ya dola milioni 950," alisema.

Dk. Nchemba aliiahidi benki hiyo kuwa serikali itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kikamilifu.

Alisema miradi hiyo inazingatia utekelezaji wa Mpango wa Tatu Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) na sehemu ya mikakati ya serikali ya awamu ya sita ya kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya wananchi.

"Mkakati huo unalenga uboreshaji wa miundombinu; upatikanaji wa nishati ya kuaminika; kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji na kuimarisha mifumo ya elimu na mafunzo. Miradi hii mitano itaongeza thamani ya miradi (portfolio) inayofadhiliwa na WB hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 5.5," alisema.

Alisema mradi wa RISE unatarajia kuboresha barabara vijijini yanayopitiwa na miradi hiyo mitano ambapo wilaya sita katika mikoa minne ambayo ni Geita, Tanga, Lindi na Iringa na itatoa ajira za watu 35,000.

Naye Warwick alisema wanaamini mradi wa RISE utawezesha Watanzania wengi wa vijijini kupata barabara za lami ili kuwezesha kupata huduma na fursa za kiuchumi.

Alisema mradi wa HEET utaongeza programu za masomo 260 katika maeneo ya shahada na zaidi ya wanafunzi 100,000 watanufaika moja kwa moja na kuimarisha taasisi za elimu ya juu 14 pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Alisema mradi wa DTP ukikamilika, zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamefikiwa na mtandao wa huduma wa simu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu alisema miradi iliyosainiwa, mmoja ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maendeleo ya barabara kwa ushirikishaji jamii na ufunguaji fursa za kijamii na kiuchumi vijijini.

## Kodi majengo kwa Luku kuanza leo

**Na Waandishi Wetu**

WAMILIKI wa majengo nchini wanaanza kulipa kodi ya majengo kuanzia leo kwa kutumia mfumo mpya wa njia ya ununuzi wa umeme kupitia mashine za Luku.

Kwa njia hiyo mpya ya ukusanyaji wa kodi, kila mnunuzi wa umeme atakatwa Sh. 1,000 kwa mwezi kwa nyumba ya kawaida na Sh. 5,000 kwa mwezi kwa kila sakafu ya ghorofa.

Kwa wale wanaotumia mita za ankara watalipa kodi hiyo kwa pamoja katika ankara ya mwezi.

Utaratibu huo unafanyika kufuatia marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 289 iliyofanyiwa marekebisho na kupitishwa na Bunge Juni mwaka huu kwa kubadili viwango vya kodi ya majengo.

Taarifa iliyotolewa jana kwa umma na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Alfayo Kidata, inabainisha kuwa wamiliki ambao majengo yao hayajapata umeme, wataendelea kulipa kodi hiyo kwa kutumia mfumo uliokuwa unatumika awali, ambao ni njia ya simu ya mkononi na benki baada ya kupata namba ya kulipia malipo mpaka hapo watakapoingiziwa umeme.

Katika taarifa yake hiyo, Kamishna Kidata alifafanua kuwa viwango vitakavyotozwa kwa sasa ni Sh. 12,000 kwa kila jengo la kawaida ndani ya kiwanja kutoka Sh. 10,000 iliyokuwa ikitozwa awali, na Sh. 60,000 kwa kila sakafu ya ghorofa kutoka Sh. 50,000.

Hata hivyo, kwa upande wa Halmashauri za Wilaya na Miji Midogo, nyumba za ghorofa bila kujali idadi ya sakafu zitatozwa Sh. 60,000.

Kamishna Kidata alisisitiza, "Utekelezaji huo unaanza rasmi Agosti 20, mwaka huu (leo) na unafanyika chini ya usimamizi wa TRA kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (TANESCO) ukihusisha mita za aina zote za umeme," alisema.

Aliongeza kuwa wamiliki wa majengo na wananchi watakaokatwa kodi hiyo kimakosa na wale watakaokuwa na malalamiko mbalimbali, watatakiwa kufika ofisi za TRA zilizoko karibu na maeneo yao kwa ajili ya kushughulikiwa.

***Imeandikwa Godfrey Mushi (ARUSHA) na Edwin Mosha (TURDACo)***

## HABARI KITAIFA

# Sabaya akiri mahakamani kumiliki silaha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa zamani wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34), amekiri mahakamani kwamba alikuwa akimiliki silaha ya moto ya aina ya Glock 17.

Ole Sabaya alikiri mahakamani huko jana kumiliki silaha hiyo wakati akikamilisha ushahidi wake mbele ya Hakimu Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Odira Amworo.

Sabaya na wenzake wawili, Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wanakabiliwa na kesi ya jinai namba 105 yenye mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha iliwakuta na kesi ya kujibu washtakiwa hao kutokana na mashtaka yanayowakabili.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, Sabaya inadai alikuwa akimiliki silaha ndogo aina ya Glock 17 na alikuwa akiitumia kwa shughuli zake binafsi hasa kwa ulinzi.

Alidai mahakamani huko kwamba silaha hiyo alianza kuimiliki Machi 24, mwaka huu.

Vilevile, Sabaya alidai mahakama huko kuwa wakati akitoka Wilaya ya Hai kwenda Arusha, alipitia barabara ya Mirerani.

Alidai hakupitia barabara ya Moshi kwenda Arusha kwa sababu alitishiwa kuuawa.

"Mimi nilikiwa kiongozi wa watu lakini nilibadilisha barabara kwa kuwa nilitishiwa kuuawa kutokana na chuki za kisiasa za Arusha na Hai," alidai.

Sabaya alidai kwamba hawafahamu mashahidi wa Jamhuri, Numan Jasin na Hajirini Saad.

Mbali na kukana kuwafahamu mashahidi hao wa Jamhuri, Sabaya pia alikana kukufika katika eneo la duka la Shaahidi Store lililoko eneo la Soko Kuu jijini Arusha siku ya tukio Februari 9 mwaka huu.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, Sabaya alidai kwamba wakati akihojiwa na Wakili wa Serikali, Tumaini Kweka, alikana kumfahamu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, marehemu Anna Mghwira, kwamba hakumbuki kama alimwapisha kwa kuwa maswali ya wakili huyo yalimchanganya, yalikuwa yamepandiana, hakumsikia vizuri na maswali hayo yalikuwa ya kumdhalilisha.

Wakili huyo wa utetezi, aliiomba mahakama hiyo kufunga kesi baada ya shahidi wa kwanza wa utetezi (Sabaya) kukamilisha kutoa ushahidi wake.

Wakili Mahuna pia alidai mahakamani huko kwamba shahidi wa kwanza hatakuwa na mashahidi wengine.




Mwakilishi wa vyama 11 visivyo na uwakilishi bungeni na Katibu Mkuu wa Chama cha ADC, Doyo Hassan, akionyesha kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katiba inayopendekezwa ya mwaka 2014, na kutaka iendelezwe hiyo na siyo kuanzishwa mchakato upya, endapo serikali itaamua kutengeneza katiba mpya. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Chama cha DP, Abdul Mluya. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Vyama 11 vya siasa vyataka serikali iitishe kura ya maoni Katiba mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MJADALA wa Katiba mpya umeendelea kuchukua sura mpya baada ya vyama 11 visivyokuwa na wabunge bungeni kuiomba serikali kuufufua mchakato wa Katiba kwa kuitisha kura ya maoni.

Vyama hivyo ni DP, NRA, ADC, AAFP, UDP, SAU, UMD, TLP, CCK, NLD na UPDP.

Vimesema mabilioni ya fedha yaliyotumika hadi kupatikana kwa Katiba inayopendekezwa hayawezi kupotea na kutaka iendelee ilipoishia.

Vyama hivyo vimetoa kauli hiyo jana mbele ya waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam.

Mchakato wa Katiba mpya ulikwama Aprili 2015 baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutangaza kusitishwa kwa kura ya maoni iliyokuwa ifanyike mwezi huo. Hatua hiyo ilitokana na kutokamilika kwa uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura.

Katibu Mkuu wa DP, Abdul Mluya, akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema: "Suala la Katiba ni suala mtambuka. Uliishia kwenye kura ya maoni na sisi msimamo wetu, tunadhani huu ni muda sahihi wa kwenda kupigia kura ya Katiba pendekezwa."

"Katiba hii pendekezwa ni nzuri, ina maoni yote ya wananchi sasa wale ambao wanataka kuturudisha nyuma wana agenda yao. Twendeni kwenye kura ya maoni na kama kuna madai mengine yataingizwa baadaye, lakini kwa sasa tuipigie kura kwanza," alisema Mluya.

Aidha, alisema hata Rais Samia Suluhu Hassan, hajatakaa uwapo wa Katiba mpya, lakini ameomba apewe muda aimarishe uchumi ambao umetikishwa na janga la corona.

"Sina hakika kama Rais amesema hataki Katiba mpya bali amesema tumpe muda ajenge nchi, kwa sasa ndio kwanza ana miezi mitano, hata katika ndoa huwezi kuonyesha dira ya familia kwa miezi mitano tu," alisema Mluya.

"Muda ukifika, badala ya kuturudisha nyuma tuendelee tulipoishia, tusije kutengeneza gharama nyingine kubwa."

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa ADC, Doyo Hassan Doyo, alisema baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa na asasi za kiraia wanatanguliza mbele maslahi yao binafsi badala ya taifa na kuwaonya kuacha tabia hizo.

Alisema kauli za kumlazimisha Rais Samia kufanya yale wanayoyataka wao si jambo zuri huku wakisema wako tayari kukutana na kiongozi huyo mkuu wa nchi ili kujadiliana kuhusu masuala mbalimbali.

Rais Samia ameweka wazi kwamba atakutana na viongozi wa vyama vya upinzani ili kujadiliana jinsi ya kuboresha demokrasia.


**bgtl** BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

*Kwa Idhini tuliyopewa* na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.**Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LAMDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAWI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SPRINT CORPORATE LIMITED/BEATUS GODBET RUGE | Kiwanja kilichopo maeneo ya Kulangwa Manispaa ya **Kinondoni,**Dar es salaam kwa jina la **Beatus Godbet Ruge** | TEGETA | 28/09/2021 |
| 2 | JOYCE GIDIONI KWAYU | Nyumba ya makazi iliyopo Vianzi, Wilaya ya Mkuranga,Pwani. | KARIAKOO | 29/09/2021 |
| 3 | NASSIR FOCUS NDESSI/THERESIA ERICK SHAYO | Nyumba yenye leseni ya makazi na. TMK041580 iliyopo Mianzini Charambe, Manispaa ya Temeke kwa jina la **Theresia Erick Shayo** | KARIAKOO | 25/09/2021 |
| 4 | MALIK SEIF SULEIMAN/ATHUMANI RAJABU JONGO | Nyumba ya makazi iliyopo Mbagala kilungule kwa nzala,manispaa ya Temeke kwa jina la **Athumani Rajabu Jongo** | KARIAKOO | 22/09/2021 |
| 5 | DISMAS FERDNAND MALLYA/ GODFREY FERDNAND MALLYA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Mbagala Kongowe kwa jina la **Godfrey Ferdnand Mallya** | KARIAKOO | 25/09/2021 |
| 6 | BAKARI SELEMANI BANYANGA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Mbagala Kilungule | KARIAKOO | 22/09/2021 |
| 7 | ERICK AMANI SWAY | i. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.**TMK/CHB/KIM2/53** iliyopo charambe mtaa wa kilungule,manispaa ya Temeke yenye Leseni na.**TMK035418** kwa jina la **Nuhu Ismail Kaitila.**<br>ii. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.**TMK/MBGL/MOR2/410** iliyopo Mbagala mtaa wa Moringe, manispaa ya Temeke yenye Leseni na.**TMK041863** kwa jina la **Juma Hamisi Kitogo** | KARIAKOO | 18/09/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**
**Email: info@bestgoup.co.tz**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**Email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

216416102

# RC awatimua watu waliojazana mochwari

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amewatimua waombolezaji waliokuwa wamefurika katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa kwa ajili ya kufuata miili ya ndugu zao.

Amesema amechukua hatua hiyo ikiwa ni udhibiti wa janga la corona ambalo linaendelea kutikisa maeneo mbalimbali ya nchi.

Sendiga akiwa ameambatana jana na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Juma Bwire, na Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alifika kwenye chumba cha kuhifadhia maiti baada ya uongozi wa hospitali hiyo kueleza kero ya wananchi kusongamana katika eneo hilo tofauti na maelekezo ya serikali. Alisema amewafukuza waombolezaji hao kwa kuwa janga la corona katika mkoa ni kubwa, hivyo lazima kila mwananchi achukue tahadhari kwa kuzingatia maagizo mbalimbali ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Waze na Watoto ikiwamo kuepuka misongamano isiyo ya lazima.

Sendiga alisema hajapendezwa na tabia ya wananchi wa Iringa pindi wanapopatwa na msiba kufika kwa wingi katika chumba cha kuhifadhia maiti kuchukua mwili. Alisema jambo hilo ni hatari na linaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa huo.

Alisema si lazima kwa wafiwa kufika kwa wingi katika chumba cha kuhifadhia maiti lakini wanaweza kufika watu wachache kufuata mwili na wengine wakasubiri nyumbani kwa ajili ya mazishi.

"Naagiza kuanzia leo (jana) watakaoruhusiwa kufika chumba cha kuhifadhia maiti kuchukua mwili ni watu wanne pekee na si zaidi ya hapo. Walinzi hakikisheni hapa nje hakuna msongamano wowote wakati wote.

"Hebu tazama hapa leo (jana) zaidi ya watu 100 wamekaa nje ya chumba cha kuhifadhia maiti na hao wamefuata mwili mmoja tu. Jiulize hawa wote wamekuja kubeba mwili huu mmoja? Hapana, haiwezekani kuacha misongamano kama hii," alisema Sendiga huku akiwataka wafiwa kuanza kutawanyika katika eneo hilo.

Pia mkuu huyo wa mkoa aliagiza ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa kutumia vyombo vya habari kuwatangazia wananchi juu ya kuepuka mikusanyiko eneo hilo la hospitali ya mkoa na maeneo mengine na idadi ya watu wanaokwenda kuchukua miili ya ndugu zao. Sambamba na hilo aliagiza ofisi hiyo kuwatangazia wananchi kwamba watu wanaokwenda kuwaona wagonjwa wasizidi wawili kwa kila mmoja.

Awali, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, alisema kumekuwapo na kero kubwa katika eneo la chumba cha kuhifadhia maiti kwa wananchi kulazimisha kuingia getini kusubiri miili ya ndugu zao.

Naye Kamanda Bwire aliagiza kampuni inayohusika na ulinzi katika hospitali hiyo, mmiliki wake kufika ofisini kwake ili kupewa maelekezo ya nini cha kufanya kwa ajili ya kuthibiti misongamano katika eneo hilo.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akizungumza na wafiwa waliofika kuchukua mwili wa mpendwa wao, katika chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa jana, ambapo aliwaamuru kuondoka katika eneo ili kuepusha mikusanyiko kwa ajili ya kukabili maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wafuasi 19 CHADEMA wafikishwa mahakamani

**Na Richard Makore,**

MWANZA

WAFUASI 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza kwa tuhuma za kufanya fujo eneo la Kanisa Katoliki Parokia ya Bikra Maria wa Madhabahu Kawekamo, jijini Mwanza.

Wafuasi hao walikamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza Jumapili iliyopita na kuwashikilia kwa siku nne hadi jana. Wote walisomewa mashtaka na Wakili wa Serikali, Gisera Alex na wakakana kutenda kosa hilo.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Emael Lukumay, Alex alidai kuwa kwa pamoja wafuasi hao Agosti 15, mwaka huu, walifanya fujo eneo la kanisa mbele ya waumini.

Hata hivyo, washtakiwa hao walipata dhamana kwa kila mshtakiwa kudhaminiwa na watu wawili wenye barua kutoka serikali za mitaa yenye picha za wadhamini, kuwa na vitambulisho vya taifa au cha mpigakura na kutia saini bondi yenye thamani ya Sh. milioni moja.

Siku ya tukio la kukamatwa wafuasi hao, walifika kanisani hapo kwa ajili ya lengo la kujumuika na waumini wengine, hususani wakilenga kumwombea mwenyekiti wao Freeman Mbowe anayesota gerezani mwezi mmoja sasa.

Mbowe alikamatwa jijini Mwanza na kusafirishwa hadi jijini Dar es Salaam kabla ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu na kusomewa mashtaka ya ugaidi.

Wafuasi hao wanadaiwa kukamatwa dakika chache baada ya kuwasili lango kuu la kuingilia katika kanisa hilo kushiriki misa.

Akizungumza na Nipashe siku moja baada ya kukamatwa, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Gideon Msuya, alikiri wafuasi hao kukamatwa mwishoni mwa wiki iliyopita jijini humo.

Msuya alidai kuwa wafuasi hao walikamatwa kwa madai ya kufanya fujo katika misa hiyo ambayo ilikuwa imehudhuriwa na waumini mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali.

Tangu Mbowe akamatwe na kuwekwa gerezani kwa tuhuma za kufanya makosa ya ugaidi, wafuasi wake wamekuwa wakimwombea katika makanisa mbalimbali hapa nchini.

Maombi ya kumwombea Mbowe yamekuwa yakifanywa na wafuasi wa CHADEMA katika maeneo mbalimbali nchini katika makanisa.

Hivi karibuni wafuasi hao walikwenda Kanisa Katoliki Parokia ya Bugando jijini Mwanza na kufanikiwa kuingia kanisani na kuomba misa maalumu kwa ajili ya kumwombea kiongozi wao.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA WAPANGAJI

1. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limepokea maelekezo ya Serikali kupitia taarifa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya utekelezaji wa ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kutumia njia ya ununuzi wa umeme kuanzia tarehe 20 Agosti, 202.
2. Tunapenda kuwafahamisha Wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwa jukumu la kulipa kodi ya majengo yake ni la Shirika. Hata hivyo, kwa kuwa Serikali imeanza utaratibu wa kulipa kodi hiyo kwa kutumia njia ya ununuzi wa umeme, tunawaomba wapangaji wetu waendelee na utaratibu huo uliowekwa na Serikali.
3. Shirika linafanya mawasiliano na mamlaka husika yaani TRA kuona jinsi zoezi hilo linavyotekelezwa ikiwa ni pamoja na kutambua wapangaji waliolipa na kiasi walicholipa na kuweka utaratibu wa namna ya kuchukua hilo jukumu bila kuathiri wapangaji.
4. Baada ya kukamilisha mawasiliano na TRA wapangaji watafahamishwa mapema ipasavyo.
5. Tunawashukuru wapangaji wote kwa kutuelewa na wanaoendelea kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kuwaletea watanzania maendeleo kwenye sekta ya nyumba.

IMETOLEWA NA:
OFISI YA UHUSIANO NA HABARI
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

216417402

# Ushahidi wa kupikwa 'wamchomoa' gerezani aliyefungwa kwa kubaka

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa Mafinga mkoani Iringa, Onesmo Makoga, ametolewa gerezani alikokuwa amefungwa maisha baada ya Mahakama Kuu kubaini ushahidi wa kubaka uliomtia hatiani ulikuwa umepikwa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Iringa mbele ya Jaji Joseph Mlyambina baada Makoga kukata rufani.

Mlalamikaji alishtakiwa kwa kubaka katika Mahakama ya Wilaya ya Mufindi kwa madai kwamba alitenda kosa hilo Agosti 26, 2017.

Mlalamikaji huyo anadaiwa kubaka mtoto wa darasa la kwanza na katika usikilizaji wa shauri hilo, alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Katika sababu za rufani, Makoga alidai kuwa Hakimu wa Mahakama ya Wilaya alikosea kumtia hatiani na kumpa adhabu hiyo kwa kuangalia ushahidi wa Jamhuri ambao ulishindwa kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

Pia alidai kuwa mahakama ilikosea kudharau utetezi wa mlalamikaji na kwamba ushahidi wa shahidi wa kwanza ambaye ni mtoto, ulikuwa wa kupandikizwa na kwamba tukio linadaiwa kutokea Agosti 26, 2017 wakati siku hiyo ilikuwa Jumamosi na watoto hawaendi shuleni na yeye alikuwa shambani.

Wakili wa Jamhuri, Alice Thomas, akijibu hoja, alidai mtoto alikuwa anakwenda katika masomo ya ziada na wakati wa usikilizwaji hakukuwa na swali kuhusu siku hiyo, hivyo hoja hiyo ya mlalamikaji ameiibua katika rufani.

Katika uamuzi wa rufani hiyo, Jaji Mlyambina alisema upande wa Jamhuri haukueleza mtoto huyo alikuwa darasa la kwanza na alitakiwa kuhudhuria masomo ya ziada.

"Nakubaliana na wakili wa upande wa Jamhuri kwamba hakukuwa na maswali kuhusiana na siku ya tukio kwamba ilikuwa Jumamosi lakini upande wa Jamhuri ulikuwa na jukumu la kufafanua kwa nini mtoto aliende katika masomo ya ziada siku ya Jumamosi.

"Siku hiyo kwa mazingira ya kawaida, wanafunzi hawaendi shuleni labda wanafunzi wanaotakiwa kufanya mtihani wa taifa kwa mwaka huo. Nakubaliana na mlalamikaji kwamba hii ni moja ya kesi ambazo ushahidi wake umepikwa. Ushahidi wa mtoto haukuwa mzuri," alisema Jaji Mlyambina.

Mlalamikaji alidai shahidi wa pili ambaye ni mama wa mtoto, alimlazimisha mwanawe kwa kumpiga ili aseme kabakwa.

Hoja hiyo ilipingwa na Wakili wa Jamhuri, ambaye alidai mlalamikaji alimfunga mdomo mtoto ili asiseme ukweli kitendo kilichomfanya mama atumie nguvu ili aseme ukweli.

Jaji Mlyambina alisema katika tukio hilo kuna mkanganyiko katika ushahidi wa shahidi wa kwanza ambaye ni mtoto na shahidi wa pili ambaye ni mama.

Katika ushahidi mtoto anadai alitolewa nje ya nyumba na mama yake akawa anamhoji wakati mama anasema alichukua fimbo akamchapa ili aseme alichofanyiwa.

"Ushahidi kama huu unaonyesha umepikwa. Ushahidi wa shahidi wa kwanza na shahidi wa pili hauonyeshi kama aliyebaka ni mlalamikaji.

"Nimeona mlalamikaji alitoa sababu dhaifu wakati anapinga kupokelewa kwa kielelezo cha maelezo yake, ushahidi wa shahidi wa nne hauungani na ushahidi wa mashahidi wengine.

"Nakubaliana na mlalamikaji kwamba Hakimu alidharau ushahidi wake wa utetezi akakubali ushahidi wa upande wa Jamhuri ukiwamo wa mtoto ambao umepikwa.

"Upande wa Jamhuri haikuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka, kutiwa hatiani na adhabu ya kifungo cha maisha aliyopewa mlalamikaji inafutwa, aachiwe huru," alisema Jaji Mlyambina.

# Serikali yafafanua vyeti kimtandao chanjo corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu utoaji vyeti vya chanjo ya corona kwa mfumo wa kielektroniki utakaoanza kutumia.

Mfumo huo unamwezesha mtoa huduma kuingiza taarifa za mteja aliyechanjwa ili kumpatia cheti.Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa ufafanuzi huo kwa waandishi wa habari.

Alisema, wizara inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 kupitia vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa nchini zaidi ya 550.

"Zoezi la utoaji wa chanjo linaendelea sambamba na utolewaji wa vyeti kwa mteja anayechanjwa," alisema Dk. Subi na kuongeza kuwa kufanikisha zoezi la utoaji wa vyeti, wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, iliandaa mfumo wa kielektroniki ambao unamwezesha mtoa huduma kuingiza taarifa za mteja aliyechanjwa ili aweze kumpatia cheti. "Pamoja na wananchi wengi kuendelea kujitokeza kupata chanjo katika vituo vyetu vilivyoainishwa, bado kuna changamoto ya upatikanaji wa vyeti kwa wateja wetu baada ya kupata chanjo.

"Changamoto hizi zimeshashughulikiwa na maelekezo kutolewa kwa waganga wakuu wa mikoa yote," alisisitiza Dk. Subi.

Alisema utaratibu wa kupata cheti hicho kwa mteja aliyefanya 'booking' kabla ni akifika kituoni mhudumu atamtafuta (Search) katika mfumo kisha atahakiki taarifa zake, kumpatia chanjo kisha kumpa cheti kupitia mfumo wa kielektroniki.

Pia, mfumo uliopo utamtumia ujumbe na 'link' ya kupata cheti cha kielektroniki kwenye simu yake ya mkononi baada ya kupata chanjo na anaweza kwenda kuprinti popote.

Alifafanua kuwa kwa mteja ambaye hakufanya 'booking' kabla watoa huduma watamsaidia kujisajili kwenye mfumo na kumpatia chanjo kisha atapata cheti chake cha kielektroniki.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA KUANDAA MPANGO KAZI WA ZIADA WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI PAMOJA NA MPANGO WA UREJESHAJI WA UWEZO WA KUJIKIMU KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)**
**KUMBUKUMBU NA: 0010006870**

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye utaalamu na uzoefu katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Ardhi imeshatwaliwa katika rasi ya Chongoleani kwa ajili ya ujezi wa kitua cha kuhifadhia mafuta kilicho pembezoni mwa bahari na kugusa jamii ambazo zinategemea ardhi pamoja na bahari ili kuweza kujikimu.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**
Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni/taasisi yaliyobobea/iliyobobea katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa uwezo wa kujikimu kwa lengo la:
- Kuandaa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) wa ziada kwa ajili ya Waguswa wa Mradi waliopo katika jamii inayoishi kwenye Rasi ya Chongoleani.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu (katika matumizi ya ardhi Pamoja na bahari) katika jamii.
- Kuandaa Mpango wa Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu (LRP) kwa ajili ya Jamii ya Rasi ya Chongoleani iliyoguswa na Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:
- Uthibitisho wa kuandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Mipango ya Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu katika miradi ya viwanda barani Afrika.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kusanifu mipango ya uhamishaji wa watu na makazi pamoja na mipango ya urejeshaji uwezo wa kujikimu katika miradi mikubwa ya ujenzi inayodhaminiwa.
- Afisa anayependekezwa pamoja na wataalam wa maswala ya ardhi na uwezo wa kujikimu katika matumizi ya ardhi na bahari pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma kwenye eneo husika.
- Uthibitisho wa usajili wa watekelezaji wa ngazi za juu katika taasisi za kitaaluma za Kitanzania au shirikisho.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili yanahimizwa.

Makampuni zenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **robin.schroh@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **25 Agosti 2021.**

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216414602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msukumo uelekezwe hamasa chanjo corona

**WAKATI** Tanzania inaendelea kutoa chanjo ya corona, kuna baadhi ya mambo ambayo yanaonekana kuwa kikwazo.

Kubwa ni kwamba kuna taarifa nyingi zinazotolewa huku zikiwa na upotoshaji mkubwa kuhusiana na chanjo hiyo. Taarifa hizo ambazo hazijathibitishwa na wataalamu wa afya, zinaibua hofu na kusababisha mwitikio mdogo wa watu kwenda kuchanja.

Serikali kwa upande wake imetimiza jukumu lake la kuwalinda raia wake, kwa kutilia mkazo suala zima la umuhimu wa chanjo ya corona, ugonjwa ambao unaendelea kuua watu wengi duniani na wengine kuugua.

Kadhalika, serikali imekuwa ikitoa kauli za kusisitiza usalama wa chanjo hiyo ambayo inatolewa bila malipo.

Kwa kadri takwimu zinavyotolewa, ni dhahiri kwamba mwitikio wa watu kwenda kuchanja hauridhishi kulinganisha na tishio lilivyo, hivyo tunaona kuwa jamii kwa ujumla iwajibike katika suala la chanjo.

Serikali isiachiwe jukumu hilo pekee kwa sababu uhai ni suala la mtu binafsi na sio la serikali. Kwa maneno mengine, wananchi wahamasishane na kuelimishana umuhimu wa chanjo na kwenda kuchanja.

Wanaokataa kuchanja kwa sababu ambazo hazina msingi, ni kikwazo kwa wengine kwa sababu ndio watakaowaambukiza wenzao.

Kadhalika, kuna kikwazo kingine kilichobainishwa kuhusu chanjo, kwamba wanawake wanaonyesha mwitikio mdogo wa kuchanja kulinganisha na wanaume. Takwimu za hivi karibuni zilizotolewa na serikali zilionyesha kuwa wanaume wanajitokeza zaidi kwenye vituo na kuchanja kuliko wanawake, ingawa sababu hazikubainishwa.

Hata hivyo, Mratibu wa chanjo, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Boniface Kitikila, amebainisha sababu za wanawake kuwa na mwamko mdogo wa kupata chanjo ya corona.

Alisema kuwa baadhi ya wanaume wanazuia wake zao kwenda kuchanjwa, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa wanawake wachache wanaojitokeza kupata huduma hiyo.

Kitikila alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi, katika semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), ambayo ilijikita zaidi kwenye elimu ya kujikinga na UVIKO-19.

Uzoefu wetu unaonyesha kuwa wanawake wamekuwa mstari wa mbele kujitokeza kuliko wanaume katika masuala ya kitaifa kama uchaguzi mkuu, sense na kampeni nyinginezo, hivyo suala la kukatazwa na waume zao nalo linahitaji kutafutiwa ufumbuzi kupitia utoaji wa elimu.

Elimu kwa jamii ndiyo njia pekee ambayo tunaamini kwamba itasaidia kuondoa vikwazo hivi dhidi ya chanjo ya corona.

Tunakubaliana na kauli ya Mkurugenzi Mtendaji wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, aliyoitoa kwenye semina hiyo kwa kuitaka jamii kuepuka kijinsia kwenye chanjo ya corona, ili kila mtu anayehitaji huduma hiyo aipate bila kuzuizi chochote, kwa kuwa ni ya bure.


Tunaamini kuwa kama kuna mwanamume anamzuia mkewe kwenda kupata chanjo ya corona, huo ni ukatili wa kijinsia, ambao haupaswi kuvumiliwa.

Tunaamini kwamba chanjo ndiyo silaha kubwa dhidi ya corona. Mambo mengine kama tiba za asili na kujifukiza ni ya ziada. Tinaikumbusha jamii kuwa corona bado ni janga kubwa.

Baadhi ya nchi kwa kutilia maanani janga hili, zimeamua kuwawekea masharti raia wake ili wachanje, ikiwamo kupata baadhi ya huduma. Tusingependa nchi yetu ifikie huko, hivyo kila mmoja alipe msukumo suala la chanjo ya corona ili kuokoa maisha yake na ya wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Miki Tasseni

# Makaa ya Mchuchuma iwe nishati majumbani

**UWEKEZAJI** kwenye mradi wa makaa ya mawe ili kuzalisha umeme unaofanywa katika machimbo ya Liganga na Mchuchuma, lengo ni kupata megawati za umeme 200 na kuongezea nishati hiyo kwenye gridi ya taifa.

Kazi hiyo ilipangwa na kutajwa kwa miongo mingi, ila baada ya kukwama nyakati hizo na kuibuliwa enzi za kuukubali kikamilifu utandawazi, tija yake katika uchumi inaingia mashakani.

Wakati huo huo, yako maeneo yanayoleta ukinzani katika kustawisha mahitaji ya jamii, ambako rasilimali hizo zingeelekezwa thamani yake, inakuwa zaidi ya miradi ya sasa.

Nyakati zilizopita hasa katika miaka kati ya 1970 na 1975 , serikali ilitaka kuanza kuwa na viwanda vya kutengeneza vipuri vya mashine za viwandani na tegemeo likawa hazina ya chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma.

Mpangilio huo ulilenga kutumia njia za kustawisha uchumi katika nchi zilizofanya mapinduzi ya ujamaa, kutoendelea na biashara ya nje inayotegemea kuanzisha viwanda kwa kuomba pesa ughaibuni au kununua nishati zao.

Matazamio ya uchumi kwa sasa ni tofauti kwani viwanda vya ndani ambavyo mashine zake na vipuri vyake huweza kutengenezwa kwa chuma cha Liganga ni kama havipo.

Labda iwe malighafi kwa viwanda vya chuma vinavyozalisha nondo, mabomba na mota ambavyo mali ghafi zake ni chuma.

Ila kinachoonekana hapa ni kuelekeza nguvu zaidi katika makaa ya mawe ambapo taasisi zimeng'ang'ana kutengeneza umeme wa kuiuzia TANESCO wakati mradi wa Stigler's Gorge au Bwawa la Julius Nyerere unatosha kwa mahitaji yaliyopo.

Pia kuna miradi mingine ya umeme wa maji ya kwenye maporomoko ya Mto Rusumo, Malagarasi na Ruhuji na kwa njia hiyo ingefaa serikali iangalie nini ambacho makaa ya mawe yanaweza kulisaidia taifa, na siyo kushadadia umeme muda wote.

Eneo ambalo lingeangaliwa tangu miaka ya 1970 lingeleta mabadiliko makubwa katika utunzaji wa mazingira na kuacha matumizi ya kuni na mkaa wa kuchoma kwa kupikia.

Kwa sababu za kitaaluma ambazo kwa njia fulani zimechanganyika na kutojituma, wataalamu eneo hilo wanasema makaa ya mawe hayawezi kutumika kupikia bila kuitoa 'phosphorus,' iliyo ndani yake.

Lakini kuna wanaosema unaweza kutumika kinachohitajiwa ni kuponda makaa hayo na yachanganywe na vitu vya ziada vinavyowaka, ili makali yake yapungue.

Ukiweka mradi wa mtaji wa taifa siyo wa kibiashara kama sehemu ya kulinda mazingira, utahitaji kununua mabaki ya mimea, vumbi randa na samadi unapata makaa yenye nguvu wastani, tena pengine kwa bei nafuu.

Suala hapa ni kuondoa matumizi ya mkaa wa unaosababisha kukata miti na kuharibu mazingira na kwa vile wilaya tofauti au halmashauri, zinazuia ukataji miti hovyo, bei ya mkaa inapanda na maisha ya kila siku yanakuwa mtihani kwa familia nyingi.

Utumiaji wa gesi ya kupikia unapigiwa debe kutokana na dhana kuwa suala hapa ni kuinua ufahamu wa jambo hilo wakati si kila familia au kaya inamudu kununua mtungi, na kuujaza mara unapokwisha.

Makaa ya mawe yanatoa njia mbadala kwa mkaa wa kuchoma, rahisi zaidi kuliko gesi, na usiohitaji fedha za kianzio za kununua mtungi au za kujaza mara inapomalizika.

Pengine ni wakati Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kuangalia namna ya kulinda mazingira kwa kuzuia kukata miti kuliko kufikiria uwekezaji kwenye umeme zaidi.

# Wastaafu walia na ucheleweshaji mafao

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WATUMISHI waliostaafu na wale wanaokaribia kustaafu, wameiomba serikali kuwalipa fedha zao mapema ili kuwasaidia kuondoa malalamiko na matatizo ya kiafya yanayoweza kuibuka baada ya kustaafu.

Rai hiyo waliitoa jana wakati wa semina na mafunzo kwa ajili ya kujiandaa kustaafu iliyofanyika jana mjini hapa.

"Mimi nimemaliza mafunzo ya kustaafu lakini ninayoyasikia kwa wezangu yananitia wasiwasi juu ya kupatikana kwa pesa zangu kwa wakati," alisema Halima Mhina ambaye alikuwa Karani wa Masijala wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Alisema ni vizuri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kulipa pesa hizo kwa wakati ili kila anayestaafu kupatiwa stahiki yake kwa kuwa hilo litaondoa malalamiko mioyoni, simanzi na kukata tamaa kwa waliostaafu na wale wanaobaki kazini.

"Tarehe ya kustaafu ya kila mtumishi inafahamika na kila upande hata PSSSF. Iweje tena malipo yachelewa? Ni wajibu wa kila upande kutimiza wajibu wake mapema," aliongeza Mhina.

"Mimi nimeondoka kazini tangu Februari 2021, lakini PSSSF nayo imekuwa goigoi kuhusu malipo yangu. Unakuja kulipwa baada ya miaka kadhaa na jambo hili linafanya mtumishi hata kupata pesa yake ya mwezi inakuwa tabu. Je, sasa ataishije?" Alihoji Malima Ndelema, aliyekuwa Mtayarishaji Mwandamizi wa Vipindi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Fedha hiyo si hisani bali ni haki ya mstaafu kwa mujibu wa sheria na kama haki inachelewa maana yake ni kuninyima haki yangu ya msingi, aliongeza Ndelema na kusema inachofanyika ni tafauti na wanayoyasema akitumia msemo wa Kizaramo kwamba: "Zilongwa mbali, zitendwa mbali."

Sambamba na kucheleweshewa mafao, watumishi hao wamelalamikia muda wa mafunzo ya kustaafu kuwa mfupi kwa kuwa wengine wanatumia wiki moja lakini taasisi zingine ni siku 21. Pia wameomba mafunzo hayo kutolewa hata kabla ya miaka mitatu ili mtumishi afanya majaribio ya mafunzo anayoyapata.



Mwenyekiti mstaafu wa Chama Kikuu cha Ushirika (RUNALI) mkoani Lindi, Hassan Mpako, akiwa katika shamba lake la alizeti hivi karibuni, ambalo anatarajia kulitumia kama shamba darasa atakapoanza kuhamasisha kilimo cha zao hilo wilayani Liwale miezi michache ijayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simu janja kutumika tiketi za mwendokasi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), umesema matengenezo ya mfumo wa kielektroniki kwa ajili kukusanya nauli (AFCS), yamefikia asilimia 80 ambapo wananchi watatumia simu janja kununua tiketi.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utendaji wa wakala kwa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Alisema kwa sasa mfumo huo umeanza majaribio tangu Julai, mwaka huu, na uhakiki wake unafanyika kwa kutumia mashine ya POS.

"Mfumo huu uko katika vituo saba ambapo watumiaji katika vituo hivyo wanaweza kununua tiketi kwa njia ya simu janja. Usimikaji na uunganishaji wa mfumo wa AFCS kwa hatua za awali unatarajiwa kuanza Oktoba, mwaka huu, wakati mfumo wa kuongoza magari wa ITS unatarajia kuanza Novemba.

"Baada ya kuwasili vifaa ambapo huduma muhimu kama kupima umbali yaliotembea mabasi wakati yakitoa huduma," alisema.

Dk. Mhede alisema mfumo huo umetengenezwa na wakala kwa kushirikiana na wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na utasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi, kujenga uwezo wa ndani kwenye mifumo ya AFCS na ITS na utaokoa gharama.

Alibainisha kuwa mfumo huo ni una uwazi katika utoaji wa taarifa za makusanyo ya nauli kuwezesha mradi kujiendesha na utatumika kwenye awamu zote sita za mfumo wa DART.

Mhede alifafanua kuwa serikali iliamua kutengeneza mfumo wake kutokana na mfumo ulioletwa na mtoa huduma UDART kushindwa kufanya kazi kutokana na mgogoro wa kimkataba na kibiashara baina yake na Kampuni ya KCC ya Ubeligiji.

"Wakala ulipokea Sh. milioni 593.97 na hadi Juni, mwaka hii, jumla ya Sh. milioni 399.82 zimetumika," alisema.

Kuhusu mchakato wa kumpata mtoa huduma, Mhede alisema zabuni inatarajia kukamilika na mkataba kutiwa sainiwa Januari 25, mwakani.

"Kwa sasa wakala ulitoa ombi la uhitimu (RFP) kwa kampuni nne zilizofanikiwa katika hatua ya awali ya ombi la sifa (RFQ) na kuendelea na hatua ya ombi la uhitimu (RFP),"alisema.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na uchache wa mabasi yanayotoa huduma ya usafiri kwa umma, Wakala inaendelea na mchakato wa kumpata mzabuni ili kuleta mabasi 95 na hivyo kukamilisha idadi ya mabasi 305.

## Ndugulile akoshwa huduma mpya NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua huduma mpya ya NMB Mkononi Plus, ambayo Waziri wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Dk. Faustine Ndugulile, ameitaja kama mwarobaini wa upotevu wa pesa na kichocheo cha kuongeza idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za bima na za kibenki kimtandao.

Uzinduzi wa huduma hiyo inayotolewa kwa wateja na wasio wateja wa NMB, ulifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Waziri Ndugulile na kushuhudiwa na Mkurugenzi wa Usimamizi na Ukaguzi wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), Neema Lutula.

Waziri Ndugulile alisema NMB Mkononi Plus ni huduma inayoakisi jitihada za benki hiyo katika kwenda na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita, ambayo imejikita katika kutokomeza foleni za kihuduma maofisini, sambamba na kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za bima na fedha kwa njia za mtandao.

"Ubunifu uendelee zaidi na NMB msiishie hapa, kwa sababu uzinduzi huu unaakisi utayari wenu katika kwenda na kasi ya Serikali, ambayo furaha yake ni kuona inaongeza idadi ya watumiaji wa bima na kutokomeza upotevu wa fedha, foleni za huduma maofisini, ambalo kwetu sisi sio jambo la sifa kamwe.

"NMB Mkononi Plus, ni mwarobaini wa changamoto za kidijitali na tunaamini unaenda kuongeza kasi ya mafanikio yenu, ambayo ni kielelezo cha ubora wa huduma zenu uliowapa tuzo mbalimbali na unadhihirisha uimara wa uongozi wa benki hii chini ya watendaji wazalendo," alisema Dk. Ndugulile.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Filbert Mponzi, alibainisha kuwa NMB Mkononi Plus ni huduma chanya kwa watumiaji wa huduma za simu za mkononi, bila kujali kama ni wateja ama sio wateja wa benki hiyo, ambayo imeanza kwa kutoa huduma tatu kubwa na muhimu.

Mponzi alizitaja huduma zilizo ndani ya NMB Mkononi Plus ni Bima Xpress (inayohusu huduma za bima), Dunduliza (inayohusisha Usajili Bima ya Afya) na Pamoja Akaunti (inayowezesha ufunguaji wa akaunti za vikundi), na kwamba huduma zaidi zitaongezwa katika mwamvuli huo kulingana na mahitaji ya wateja na wasio wateja.

"Leo hii kupitia NMB Mkononi Plus, tunathibitisha ubora na ubunifu tulionao, tunaosema kila uchao. Mkononi Plus ni ya wote, wateja na hata wasio wateja wetu, hii ni tofauti na ile huduma ya NMB Mkononi, ambayo ni maalum kwa wateja tu na sio zaidi.

"Wito kwa wateja ni kuwataka kuendelea kupata huduma bora na rafiki zitolewazo NMB, na wasio wateja wetu, tunawaomba waungane nasi kuhudumiwa na benki yetu, ambayo imeshinda tuzo kadhaa za kitaifa na kimataifa, huku tukijivunia kuwa wabunifu wa masuluhisho mbalimbali kupitia uwekezaji mkubwa wa kidijitali tuliofanya," alisisitiza Mponzi.

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi na Ukaguzi TIRA, Neema Lutula, aliipongeza NMB kwa ubunifu uliozaa huduma hiyo, anayoamini itakuwa chachu ya kuongeza idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za bima, ambao kwa sasa ni wachache.

"Sisi kama wasimamizi na bima nchini, tumefurahishwa na ujio wa NMB Mkononi Plus, tukiamini unaenda kuchagiza watu wa kada zote kutumia huduma za bima na wito wetu kwa benki ni kuimarisha mahusiano mema na ushirikiano chanya na kampuni za bima nchini, ili kurahisisha utoaji huduma kwa Watanzania," alisema Lutula.

# TIC, ZIPA kushirikiana kukuza uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) zimetia saini mkataba wa kushirikiana kwenye maeneo 12 ya kuhamasisha uwekezaji nchini.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana kwenye ofisi za TIC jijini Dar es Slaam baina ya Mkurugenzi Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Maduhu Kazi na Mkurugenzi Mkuu wa ZIPA, Shariff Ali Shariff.

Akizungumza kuhusu makubaliano hayo, Dk. Kazi alisema miongoni mwa makubaliano hayo ni kutangaza vivutio vya utalii kwa pamoja na kushiriki kwenye maonyesho mbalimbali.

Dk. Kazi alisema watakuwa wakishirikiana kwa kupeana taarifa mbalimbali za uwekezaji na kushiriki matamasha ya kuhamasisha uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema kwenye makubaliano hayo, pia watashirikiana kufanya utafiti mbalimbali ambao ni muhimu kwa uwekezaji na kubadilishana taarifa, ujuzi na uzoefu kwa masuala ya shughuli hiyo,

"Kuna maeneo ambayo wenzetu ZIPA wako mbele, hivyo tutachota uzoefu wao na sisi kuna maeneo ambayo wanaona tumeenda mbele kuliko wao, hivyo watapenda tuwape siri ya mafanikio ili nao wafikie mafanikio hayo," alisema

Dk. Kazi alisema hata kabla ya kutiwa saini kwa ushirikiano huo, kumekuwa na mambo ambayo tayari wameshaanza kushirikiana yakiwamo maonyesho ya kimataifa ya biashara yaliyopita ambapo walikuwa kwenye banda moja.

Alisema kwa mujibu wa mkataba huo, kutakuwa na uwezekano wa kuongeza mambo mengine zaidi ya hayo 12 iwapo wataona kuna haja ya kufanya hivyo na kwamba hilo litawezekana baada ya pande zote kuridhia ongezeko hilo.

Pia alisema kuna kamati ya pamoja ambayo itaratibu ushirikiano huo ambayo itakuwa na jukumu la kukumbusha wajibu wa kila upande na kama kuna kasoro itashauri cha kufanya.

"Tutafanyakazi pamoja mfano TIC ikienda kwenye maonyesho ambayo ZIPA haipo basi itawajibika kuelezea vivutio vyake na pia kufanyakazi ya ZIPA kuelezea vivutio vinavyopatikana Zanzibar," alisema

Shariff kwa upande wake alisema ushirikiano baina ya taasisi hizo utakuwa na manufaa makubwa kwenye sekta ya uwekezaji kwa upande wa Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema kutakuwa na siku ya uwekezaji kila mwaka ambayo itakuwa ikifanyika kwa kupokezana baina ya Tanzania Bara na Visiwani.

Shariff alisema moja ya majukumu yao yatakuwa kuzishauri serikali kuondoa sheria na taratibu ambazo zitaonekana kuwa kikwazo kwa uwekezaji kwa pande zote mbili.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (katikati), akikata utepe kuashiria kukabidhiwa vyoo vipya vya kisasa vilivyojengwa na Rotary Klabu ya Bahari ya Dar es Salaam katika Shule ya Sekondari Mtakuja, Kunduchi Beach mkoani humo jana. Wengine ni Rais wa Klabu hiyo, Diamond Carvalho (wa tatu kulia), Diwani wa Kata ya Kunduchi, Michael Urio (wa nne kulia), Mwenyekiti wa Bodi wa Shule, Mary-ani Lema (wa nne kushoto), Mkuu wa Shule, Magdalena Matiku (wa tatu kushoto) na wadau mbalimbali wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka hamasa urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta,**

DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi nchini kutumia njia mbalimbali katika kuhamasisha urasimishaji ili kuongeza kasi ya utoaji hati.

Dk. Mabula alisema hayo juzi katika kikao cha watendaji wa sekta ya ardhi, kampuni za upangaji na upimaji kilichofanyika katika Chuo cha Mipango, jijini hapa. "Tunahitaji kuhamasisha urasimishaji na tunaweza kushirikisha taasisi za siasa ili zisaidie kazi hiyo," alisema.

Wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi mkoani Tabora hivi karibuni, Dk. Mabula alitembelea ofisi ya Chama cha Mapinduzi Mkoa na kuelezwa na Mwenyekiti wa Mkoa, Hassan Mwakasubi, kuwa wako tayari kusaidia uhamasishaji wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na hatimiliki ya ardhi.

Alisema taasisi za kisiasa zinaweza kusaidia kuhamasisha wananchi kumilikishwa ardhi badala ya kuiachia serikali pekee kwa kuwa mara nyingi taasisi hizo zimekuwa karibu na wananchi.

"Tunapozungumzia urasimishaji isiwe suala la hiari. Ni vizuri tukawaeleza wamiliki faida na kipi kinawafanya wafurahie umiliki wa ardhi," alisema Dk. Mabula.

Pia aliwaambia watendaji hao waliojumuisha makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa na wasajili wa hati na nyaraka kuwa ni vizuri wakati wa uandaaji hati wakawekeana malengo ili kutoa hati nyingi na kusisistiza kuwa viwanja vyote vilivyoidhinishwa ni lazima viandaliwe hati.

Awali, akizungumza na watendaji hao, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema uhamasishaji lazima ufanyike ili wananchi wajue kama wanapaswa kuingia kwenye suala hilo na kuelewa umuhimu wa upatikanaji miundombinu.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kwa sasa umiliki wa ardhi katika maeneo ya mijini ni suala la lazima na wananchi wenye nyumba au viwanja wanatakiwa kuchangamkia urasmishaji.

# Diwani ahimiza chakula shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZAZI na walezi katika Kata ya Kongowe Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wametakiwa kutilia mkazo suala la chakula shuleni ili kuwawezesha watoto kuwa na utulivu darasani na kufanya vizuri katika masomo yao.

Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari, alisema jana kuwa pamoja na maagizo yanayotolewa na viongozi, bado kikwazo ni kwa wazazi kuwapatia watoto fedha za chakula shuleni.

Shomari alisema uwapo wa chakula shuleni unawafanya wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao na kuinua ufaulu katika kata hiyo na mkoa kwa ujumla.

"Mtoto hawezi kusoma akiwa na njaa na katika kata yangu waliofanikiwa kupata chakula shuleni ni wanafunzi wa darasa la nne na la saba ambao wazazi wao wanajitahidi kuwa na mwamko wa kuwapatia watoto wao fedha za chakula wawapo shuleni," alisema Shomari.

Alisema kubwa haja kwa wananchi kupatiwa elimu ya umuhimu wa chakula shuleni kwa wanafunzi na madhara yake ili wajitoe kwa namna wanavyoweza kutoa fedha za chakula kwa watoto wao.

Shomari alisema hali duni kwa baadhi ya wazazi pia ni kikwazo kinachosababisha washindwe kuwapatia watoto wao fedha za chakula.

"Kwenye kata yangu kuna kikwazo cha wanafunzi kupata chakula shuleni, wazazi wengi wanakwama kutoa fedha kwa watoto wao, utakuta kwenye watoto 100 wanaokula ni 40. Hao wengine hawapati chakula," alisema.

Naye Diwani wa Mailimoja, Ramadhani Lutambi, alisema katika kata yeke watoto wanaopatiwa fedha za chakula shuleni idadi yao ni ndogo kulinganisha na uhalisia.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwataka viongozi wa halmashauri zote na watendaji wa afya kitengo cha lishe mkoani hapo kuhakikisha chakula kinapatikana shuleni.

Alisema hali ya udumavu kwa mkoa huo ni asilimia 23.8 kulinganisha na ya taifa ambayo ni asilimia 30.1.

" Tafsiri yake ni kuwa katika watoto 100 wenye umri chini ya miaka mitano watoto 24 wamedumaa na katika kila darasa lenye watoto 45 watoto 11 wanaweza kuwa wadumavu na hawafundishiki, hivyo basi ni vyema tukaona umuhimu wa kusisitiza upatikanaji wa chakula shuleni," alisisitiza

Kunenge alishauri shule kuzalisha matunda, mboga na mazao ya chakula kama vile mihogo, mahindi na mpunga pia ufugaji wa wanyama wadogo kama kuku, bata na sungura kulingana na hali halisi ya eneo la shule.

# MeTL yajitosa kulinda ajira kwa vijana nchini

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KAMPUNI ya Mohammed Enterprises Ltd (MeTL), imeamua kurejesha fadhila kwa wateja wake kwa kutoa huduma za kurekebisha bajaji zaidi ya 1,500 ili kuboresha mapato kwa vijana nchini.

Mwakilishi wa MeTL, Zakayo Edward, ambaye ni muuzaji wa bajaji hizo nchini na Afrika kwa ujumla, alisema jana mjini hapa kuwa hiyo ni sehemu ya uwajibikaji wa kijamii (CSR) unaofanywa na MeTL.

Alisema kuwa katika utafiti mdogo walioufanya, wamebaini madereva wengi wa bajaji hawafikirii hali ya bajaji zao na kuzifanyia marekebisho kwa wakati.

"Ni lengo la MeTL kupitia CSR ni kutoa huduma kwa bajaj 1,500 kote nchini, ambazo ni RE4s na Maxima ili kuzipa ubora na kuzalisha mapato ya vijana wa Kitanzania wanaokabiliwa na kero ya ukosefu wa ajira," alisema.

Alitaja idadi ya bajaj ambazo tayari zimepatiwa huduma ni pamoja na Mkoa wa Iringa 200, Dodoma 250 wakati 500 Kanda ya Ziwa, Kigoma 150, Morogoro 150, Arusha 150, Dar es Salaam 300 na Kilimanjaro 200.

Alisema hivi karibuni kampuni hiyo itatoa bajaji zenye ubora zaidi ya zilizopo ambazo zitakuwa na redio na mnara wa kusoma matumizi ya mafuta na mwendo sambamba na ubora wake kwa kuwa na injini inayoendesha kilomita 4,000 kwa mafuta kidogo.

Ofisa Masoko wa Ukanda wa Kati, Kenny Mwangosi, alitoa wito kwa wamiliki kuzingatia aina ya bajaji na asili ya barabara ili kuzifanya bajaji zao kubaki katika ubora wake katika muda uliopangwa kwa matumizi.

Alisema bajaji aina ya Maxima ina malengo mengi kwa kuwa inachukua abiria saba huku ikiwa na injini yenye nguvu hata ya kupandisha kwenye milima wakati RE4s inachukua abiria wanne ikiwa na uwezo mzuri wa kutembea maeneo tambarare zaidi.

"Ingawa wengi wanapendelea RE4s kwa sababu ya matumizi ya mafuta lakini huchukua abiria wachache kuliko Maxima na hivi karibuni kampuni itasambaza bajaji ya kisasa ambayo inafuta udhaifu wote wa bidhaa mbili," alisema.

Mmoja wa wamiliki wa bajaji, Juma Ahmad, ambaye pia ni dereva wa bajaji zinazofanya safari mjini, aliishukuru kampuni ya MeTL kwa msaada wao huo.

Alisema kuwa mbali na kuwapa msaada huo, wamewaelimisha na kuona umuhimu wa huduma kwa wakati katika bajaji zao.

Alisema wameelimika na kujua kuwa suala la umwagaji mafuta kila baada ya wiki mbili linapaswa kwenda sambamba na kuondoa vifaa vilivyochoka ili kuboresha mfumo mzima wa bajaji.

# Maziwa yasiyo na viwango yakamatwa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

BODI ya Maziwa Tanzania (TDB) imefanya msako maalum katika maduka mbalimbali jijini Dodoma na kukamata maziwa yasiyo na viwango, yaliyoisha muda wake na yameingizwa nchini bila vibali.

Aidha, imetenga kiasi cha Sh. milioni 200 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vinne vya kisasa vya kukusanya maziwa.

Akizungumza jana na Nipashe, Msajili wa bodi hiyo, Dk. George Msalya, alitaja aina za maziwa yaliyokamatwa na kuondolewa sokoni kuwa ni pamoja na Nura, KCC, Brookside, Aptamil, NIDO Forti Croissance, Cow &Gate na SMA PRO.

"Serikali imeruhusu wafanyabiashara kuingiza bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi kwa sababu mbalimbali za msingi, lakini wafanyabiashara wanapaswa kufuata utaratibu na sheria zilizowekwa ili kuweza kuagiza na kuuza maziwa yanayokidhi vigezo na viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO)," alisema.

Alisema bodi haitawafumbia macho baadhi ya wafanyabiashara wanaokosa uzalendo kwa kiwango cha kuingiza maziwa feki kwa njia za panya kwani hali hiyo inahatarisha maisha na afya za walaji.

"Maziwa haya, mengi huwa yanaingizwa nchini kwa njia ya bandari bubu ya Handeni Tanga, hali ambayo inaikosesha pia serikali mapato," alieleza.

Alisema, kwa mujibu wa sheria, wafanyabiashara hao waliokamatwa na bidhaa hizo watatozwa faini kati ya Sh. milioni 2.5 na Sh. milioni 5, pamoja na hatua nyingine za kisheria.

"Pamoja na adhabu hizo, bodi inaendelea kuwakumbusha na kuwaelimisha wafanyabiashara wote wanaotaka kuingiza bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi kufuata taratibu za kisheria zilizowekwa na serikali ili kuepuka usumbufu na pia, kuhakikisha Watanzania wanatumia maziwa yaliyokidhi viwango vya afya," aliongeza.

"Ninawaomba sana wafanyabiashara na wawekezaji wengine wote wa sekta ya maziwa kutaka vibali na ushauri kutoka Bodi ya Maziwa na mamlaka nyingine, ikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS)," alisisitiza.

Kuhusu vituo vya kukusanya maziwa, alisema vituo hivyo vinatarajiwa kujengwa katika Wilaya za Mkuranga, Rufiji, Kisarawe mkoani Pwani na Karagwe mkoani Kagera.

"Tunatarajia kutekeleza mradi huu kwa ushirikiano na Wizara ya Mifugo kwa lengo la kuhakikisha tunakusanya maziwa ya kutosha kutoka kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika maeneo husika."

Alisema bodi inaendelea na jitihada za kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kujenga vituo vingi vya kukusanya maziwa katika maeneo yote ya nchi yenye shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ili kuhakikisha viwanda vya kuchakata maziwa vinapata malighafi ya kutosha.



Rais wa Mahakama ya Afrika na Haki za Binadamu, Jaji Imani Daud Aboud, akiongoza wafanyakazi wa mahakama hiyo kuchanja chanjo ya UVIKO-19, jijini Arusha mapema wiki hii. Chanjo hiyo iliwahusu wafanyakazi wa mahakama hiyo wanaoishi Arusha wakiwamo wa PAPU na AUABC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko: Wizi wa madini umedhibitiwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema serikali ipo makini katika kudhibiti wizi wa madini, na kwamba hakuna hata mtu atakayethubutu kuiba hata jiwe moja na kwenda nalo Ulaya.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kalungu Wilaya ya Momba mkoani Songwe, baada ya kutembelea kuona shughuli za utafiti wa gesi ya Helium, unaofanywa na kampuni ya Helium One ya Norway katika kijiji cha Kamsamba.

Hatua ya Biteko kutoa kauli hiyo ilifuatia madai ya wananchi kwamba kuna watu wanabeba viroba vya madini na kuondoka navyo, hivyo kuingiwa na hofu kuwa utajiri wa madini unaibwa.

"Kuna watu wanatengeneza hadithi, RC (Mkuu wa Mkoa) amezungumza hawa watu wanafanya utafiti, niwahakikishie hakuna mtu ataiba hata jiwe moja akaenda nalo Ulaya, Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ipo kuhakikisha madini yanaongezwa thamani na kuleta uchumi wa wananchi," alisema.

Biteko alisema Tanzania ni nchi ya nne kwa Afrika na ya 18 duniani kwa kuwa na madini mengi na ya pili katika Afrika kwa kuwa na madini ya vito, hivyo Rais Samia anataka kuona utajiri wa madini unawanufaisha Watanzania.

"Leo tunazungumzia Helium, hakuna Afrika nzima na nchi yenye gesi ya Helium isipokuwa Tanzania tu, nchi zinazozalisha Helium ni Marekani, Urusi na Qatar," alisema.

Alisema madini ya Helium yatakapoanza kuchimbwa utajiri wa watu utaanza kuonekana na kuwataka wananchi kazi yao kubwa iwe ni kuwapenda wawekezaji na sio kuwachukia.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema kampuni inayofanya utafiti wa helium katika bajeti ya mwaka huu wamepanga kutoa Dola za Kimarekani 25,000 kwa ajili ya kusaidia uboreshaji wa miradi ya maendeleo katika kata nne zinazozunguka mgodi.

Mgumba alisema serikali imeendelea kuujali Mkoa wa Songwe ambapo imeshaleta zaidi ya Sh. bilioni 43 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati kwenye vijiji vyote vya mkoa huo.

Kwa upande wake Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe, alimshukuru waziri kwa msaada aliotoa wa shilingi milioni tano alizochangia kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya Kamsamba na Kalungu.

# Chanzo halmashauri kupata hati chafu hiki

**Na Anthony Ishengoma**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, ameyataja mawasiliano hafifu kati ya ofisi za halmashauri na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuwa moja ya chanzo kilichosababisha baadhi ya halmashauri mkoani Shinyanga kupata hati chafu na zenye shaka.

Hati hizo zilitolewa na ofisi ya CAG mwaka wa fedha 2020 baada ya ukaguzi.

Dk. Philemon Sengati aliongeza kuwa halmashauri hizo zilishindwa kufanyia kazi baadhi ya hoja mpya, ambazo awali hazikuwamo katika hoja za ofisi ya CAG, lakini halmashauri zikashindwa kuzijibu kwa wakati na kusababisha baadhi ya halmashauri kupata hati chafu na zenye shaka.

Alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2021, na kuahidi kuwa mkoa utahakikisha kasoro zilizojitokeza na kusababisha halmashauri kupata hati chafu na zenye shaka hazitokei tena.

Dk. Sengati aidha, aliitaja sababu nyingine ni wahasibu kukosa mafunzo ya ufungaji hesabu za serikali ikiwamo namna bora ya uandishi wa taarifa ya hesabu za serikali na kuongeza kuwa mkoa utahakikisha wanahesabu hao wanapata mafunzo hayo mara kwa mara, kwa lengo la kuboresha ufanisi wao katika kufunga hesabu za serikali.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Shinyanga, Mlolwa Mabala, aliutaka uongozi wa Mkoa kuhakikisha Halmashauri za Shinyanga hazipati hati chafu kwa kuwa suala hilo haliletei sifa nzuri kwa mkoa.

Ni katika uchangiaji wa taarifa hiyo Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, wakati akichangia suala la afya Mkoani humo alipoomba ufafanunuzi kuhusu suala la wanaume kuongozana na wenzi wao kwenda kliniki kwani kwa mila za Kisukuma suala hilo linaenda kinyume cha utamaduni wao.

Akitoa ufafanunuzi juu ya suala hilo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema lengo la serikali ni kuongeza upendo kwa wanandoa, pia ni kumfanya mwanaume atambue magumu na machungu ambayo mama anayapitia ikiwamo suala zima la kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).




Mkurugenzi wa Mikakati na Ukuaji wa Kampuni ya Coca-Cola Kwanza, Josephine Msalilwa (kushoto), akimkabidhi ufunguo wa pikipiki ya magurudumu matatu mmoja wa wasambazaji wakubwa wa vinywaji wa kampuni hiyo, Silvanus Swai, baada ya kutambua mchango wake katika mauzo ya bidhaa hiyo, jijini Dar es Salaam, juzi. Kampuni hiyo, imewazawadia wafanyabiashara waliofanya vizuri katika kipindi cha miezi minne iliyopita kama motisha wa kuendelea kufanya vizuri. Kulia ni Mkurugenzi wa Mauzo wa kampuni hiyo, Eric Ongara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge waelezwa msimamo wa marufuku utafiti mbegu za GMO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameelezwa kuwa msimamo wa serikali juu ya kupiga marufuku utafiti wa mbegu zilizoongezewa vinasaba (GMO), upo pale pale licha ya kusisitiza ulazima wa kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mbegu nchini.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wabunge katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilipokutana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Prof. Mkenda alifafanua suala hilo kufuatia hoja ya Mbunge wa Kuteuliwa, Dk. Bashiru Ally aliyetaka kujua msimamo wa serikali kwenye matumizi ya GMO.

Alisema kuwa katika ulimwengu wa sayansi kuna msuguano mkubwa wa usalama wa kiafya kwa wanadamu kula vyakula vilivyotokana na mbegu za GMO.

"Tatizo kubwa la matumizi ya mbegu hizi ni kuiongezea utegemezi mkubwa wa mbegu ilhali taifa lipo katika mkakati wa kuhakikisha linaongeza uzalishaji wa mbegu ndani ya nchi," alisema.

Alisema hakuna sababu ya kuagiza mbegu nje ya nchi kwa kuwa kuna ardhi nzuri yenye udongo wenye rutuba kwa ajili ya mazao.

"Hivyo wajibu wetu ni kuhakikisha TARI inaendelea kufanya utafiti wa kina na Mamlaka ya Mbegu (ASA) kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo kuzalisha mbegu bora na kwa wingi," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Dk.Christine Ishengoma, alipongeza msimamo wa serikali kwa hatua ilizozichukuliwa kwenye GMO.

"Tunapongeza namna vituo vya utafiti vimekuwa vikifanya kazi kwa karibu na wananchi na kuitikia wito wa wabunge katika masuala ya kilimo na kuiomba serikali kuongeza uzalishaji wa mbegu husussani za alizeti na tunapongeza ASA kwa kuja na mbegu ya alizeti ambayo imeonesha mafanikio makubwa," alisema.

Mwaka 2018, serikali iliagiza TARI kusitisha mara moja shughuli za utafiti wa mbegu za GMO pamoja na kuteketeza mazao yote yaliyokuwa yakitumika kwa ajili ya utafiti.

Hatua hiyo ilitokana na wizara hiyo kujiridhisha kuwa taasisi hiyo ilikuwa imeshaanza kutangaza matokeo ya utafiti kabla ya kuthibitishwa na serikali.

# Sababu wanawake kutochangamkia chanjo corona hii

**Na Yasmine Protace**

MRATIBU wa Chanjo Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Boniface Kitikila, amebainisha sababu za wanawake kuwa na mwamko mdogo wa kupata chanjo ya corona.

Amesema idadi kubwa ya watu wanaojitokeza kupata huduma ya chanjo ya corona ni wanaume.

Bila kutaja idadi, mratibu huyo amesema, baadhi ya wanaume wanazuia wake zao kwenda kuchanjwa, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa wanawake wachache wanaojitokeza kupata huduma hiyo.

Kitikila alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi, katika semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), ambayo ilijikita zaidi kwenye elimu ya kujikinga na UVIKO-19.

"Hakuna anayejua ugonjwa utaisha lini, serikali inataka watu wake wawe salama, lakini kwenye manispaa yetu, idadi kubwa ya wanaojitokeza kuchanjwa ni wanaume," alisema Kitikila.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alitaja jamii kuepuka kijinsia kwenye chanjo ya corona, ili kila mtu anayehitaji huduma hiyo aipate bila kuzuizi chochote, kwa kuwa ni ya hiari.

"Chanjo ni hiari ya mtu, hivyo ukatili wa kijinsia usitumike kwa baadhi ya wanaume kuwazuia kinamama kwenda kupata chanjo, kwani huduma hiyo ni ya hiari," alisema Liundi.

# Waziri agawa vifaa vya TEHAMA shuleni

**Na Paul Mahundi,** MASASI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), ambaye ni Mbunge wa Masasi Mjini, Geoffrey Mwambe, kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) amegawa kompyuta tano na vifaa vingine kwa shule nne za sekondari.

Vifaa hivyo ni monitor, extension cable, printer na spika kwa shule za Mtandi, Masasi kutwa, Marika na Mtapika zilizoko katika jimbo hilo.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mwambe, Katibu wa Mbunge huyo, Imani Mkumbo mbali ya kuipongeza UCSAF kwa kumuunga mkono mbunge, alisema vifaa hivyo ni miongoni mwa juhudi zinazofanywa na mbunge katika kuhakikisha sekta ya elimu inaimarika jimboni hapo ikiwamo kuzingatia nyakati zilizopo za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Alisema lengo la mbunge ni kuona na kuhakikisha vijana wengi wakifanikiwa kwenye elimu na kuwataka wanafunzi hao kuvitunza na kuvitumia vifaa hivyo kwa umakini mkubwa ili viweze kutumiwa na wanafunzi wengine wengi zaidi.



**VIJANA WAIOMBA SERIKALI...**

Tunataka kuwa sehemu ya mpango huu wa maendeleo

Ukurasa 14



## Huu ndiyo utitiri wa utajiri ndani ya uchumi wa bluu

Ukurasa 12



# Wanawake wauza dagaa DRC waeleza wanakwamishwa wapi

**Na Mwandishi Wetu**

LINAPOKUJA suala la uwekezaji na ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wanawake wa Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, wana mchango wa kipekee.

Ni kwa sababu ndiyo wahusika wakuu wa biashara ya samaki, wakiwauza dagaa mchele wakavu kwa muda wote wafanyabiashara kutoka DRC.

Dagaa hao wako wa aina mbili wanaochemshwa na chumvi na kukaushwa juani maarufu kama dagaa nyama, lakini pia wapo wengine wanaokaushwa kwa jua na kuuzwa bila kuchemshwa na chumvi kwanza kama walivyo wengine, wakiitwa dagaa wa baharini.

Kina mama hawa wanazungumza na Nipashe wakisema uchuuzi huo wa dagaa unaofanywa na wanawake karibu kila nyumba ya Kilwa una walakini kwa sababu unaonekana kama haumnufaishi mwanamke wa Kilwa.

Kwa mujibu wa maelezo yao hakuna kikubwa cha kujivunia. Faida ni kiduchu wanasema ndiyo maana kwa miongo mingi wameuza dagaa lakini nyumba zao ni za makuti na viwango vya maisha viko chini.



Fatuma Machalila, mchuuzi wa dagaa tangu 1993, anayesema mambo ni magumu biashara hailipi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

**WANAKWAMA WAPI?**

Fatuma Machalila, anasema tangu 1993 anauza dagaa kwa wafanyabiashara Wakongo lakini kinachomkwamisha ni soko, mtaji na kiteknolojia ya ukaushaji na mbinu za kuboresha biashara hiyo.

Fatuma anasema kuuza dagaa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wake, "Kazi hii ya kuuza dagaa ni ya wanawake karibu wote wa Wilaya ya Kilwa. Kila mmoja nyumbani kwake lazima kuna vichanja vya kuanika dagaa na mteja wetu mkubwa na wa uhakika ni Mkongo kwa upande wa nje ya mipaka, lakini pia tunao wengine kutoka, Tandahimba na Masasi japo hachukui shehena kubwa,"

Anamtaja Mkongo ndiye mteja mama lakini ananunua kwa bei anayoitaka. Ni kwa sababu ndiye anayezungumza nao na kuwapa pesa za kununulia dagaa anazohitaji.

Anasema, "hatuna mitaji, mfanyabiashara huyo ndiye anayeleta pesa kwetu na kuagiza aandaliwe kiasi anachotaka. Tunapata faida kidogo kwa sababu biashara haianzii kwetu ni mpaka afike na fedha. Kila kitu hakikui, nyumba ni za makuti wala kipato hakiongezeki, "anasema Fatuma.

"Mkongo ndiye mteja mkuu ananunua bei anayoitaja. Sisi tunanunua ndoo moja ya dagaa mchele Shilingi 20,000 lakini wakati wa upepo inafikia Sh.50, 000. Kwa bei ya kawaida naweza kununua kati ya ndoo 100 hadi 200. "

Anasema ukichemsha wanapungua zaidi na waliochemshwa ndoo ya lita 10 huuzwa Sh.50, 000 wakati zisizochemshwa bei yake ni Sh. 35,000 kwa kipimo hicho.

**SOKO NI TATIZO**

Mayasa Kasie ni mchuuzi anayesema mbali na soko la DRC wachuuzi wa dagaa hawana jingine la uhakika mara nyingi wanaitegemea nchi hiyo na kwamba licha ya kuuza Ruangwa, Masasi na Tandahimba, hakuna maeneo mengine ya uhakika.

Anataja teknolojia ya ukaushaji kuwa ni duni inategemea jua muda wote na wakati wa masika, hawana namna ya kuwakausha.

Mbali na kukosa soko la uhakika, mitaji na teknolojia wanasema serikali haijaboresha biashara hiyo licha ya kwamba ni chanzo kikuu cha mapato ya Kilwa na taifa.

Wanasema dagaa wanakaushiwa nyumbani kwenye vichanja vya kienyeji na kuanuliwa jioni.

Wanaeleza kuwa ukataji miti kupata kuni za kukaushia dagaa ni changamoto kwa vile si nishati endelevu. Wanaomba serikali kusaidia upatikanaji wa nishati rafiki mbadala wa mazingira.

**WANACHOTAKA**

Wanatamani kuwa na kiwanda cha kuchakata, kufungasha sehemu za kuwakausha za teknolojia ya kisasa wakati wote bila kujali msimu wa masika.

Wanatamani kupata mafunzo ya elimu ya biashara na uwekezaji kitaalamu na mitaji ya kutosha angalau milioni 15 kwa kila mmoja, licha ya kuwapo mikopo ya kinamama, vijana na wenye ulemavu inayotolewa na halmashauri.

Fatuma anasema wanajua umoja ni nguvu na wameshaunda chama cha ushirika cha wanawake wachakata mazao ya baharini wilaya ya Kilwa, chenye wanachama 350, tangu mwaka 2019.

Pamoja na kukamilisha taratibu zote kinachowakwamisha ni kukosa usajili, licha ya kufanya juhudi nyingi.

Nipashe inazungumza na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kilwa, Abushir Mbwana, kuhusu hoja za wajasiriamali hao, anayesema soko la dagaa liko wazi wanaweza kuuza popote na serikali haijaweka kizuizi.

Akijibu suala la teknolojia na ukaushaji mbadala wa kuni, Mbwana anasema maofisa uvuvi wamewafundisha kinamama hao teknolojia ya kisasa, lakini mara nyingi imekuwa vigumu kuipokea na kuendelea na ile waliyoizoea.

Anawataka kuwasiliana na ofisi ya ushirika wilayani hapo na kukamilisha usajili wa chama cha ushirika jambo analosema linawezekana na hakuna vipingamizi iwapo wamefuata na kukamilisha taratibu zote.

Anawashauri kujiunga na kuwekezaji kwenye miradi ambayo itakuwa na tija zaidi na kuboresha biashara hiyo.

UCHUMI

# Huu ndiyo utitiri wa utajiri ndani ya uchumi wa bluu

**Na Ester Mgidula**

MAJI yanayotumiwa duniani yakiwamo ya mvua, mwenendo wa hali ya hewa , mazingira na muhimu zaidi hewa ya okisjeni wanayovuta binadamu na ile ya ukaa wanyama na binadamu wanayotoa mfumo wake unarekebishwa na bahari.

Bahari ni kama mama wa dunia kwa hiyo ulinzi wake na matumizi endelevu ya rasilimali zilizo ndani yake ni lengo namba 14 la malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) likiihamasisha dunia kulinda na kuendeleza afya ya eneo hilo.

Wataalamu wa elimu bahari wanasema ustawi wa bahari na rasilimali zake ni muhimu kwa afya ya binadamu hivyo ni muhimu kulinda isichafuliwe na taka sumu, ngumu, uvuvi wa uharibifu na wa kumaliza samaki, uchafuzi wa bahari na kuongeza kemikali za sumu eneo hilo.

Katika kulinda bahari , wananchi wanategemea kuvuna na kunufaika na rasilimali zilizomo majini kupitia dhana mpya ya uchumi wa bluu au uchumi wa bahari kuu , ambayo ni mada inayoanza kusikika kwenye masikio ya watu wengi zama hizi , lakini huenda wenye uelewa mzuri si wengi.

Hivi karibuni, Zanzibar imeanza mikakati ya kutekeleza miradi ya uchumi wa bluu, iliyoanza kwa kuunda Wizara ya Uchumi wa Bluu na Maendeleo kushughulikia eneo hilo na kusimamia uvuvi wa bahari kuu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi anapochukua uongozi anaahidi kuboresha sekta hiyo na kusema uchumi huo unafunganisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki na ujenzi wa viwanda vya samaki.

Anataka pia ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini na wizara hiyo imeonyesha njia katika mchakato wa kuboresha mazingira ya wananchi kufanya biashara na kukuza uchumi wao kupitia sekta ya maji.

**UCHUMI WA BLUU NI NINI ?**

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk.Tumaini Gurumo, anasema dhana ya uchumi wa bluu inajumuisha uwekezaji kwenye uvuvi na ufugaji baharini pamoja kilimo na ujenzi wa viwanda wa kuchakata bidhaa za baharini.

Dokta Gurumo anatoa ufafanuzi huo kwenye warsha iliyohudhuriwa na wanahabari jijini Dar es Salaam, inayolenga kuhamasisha na kuufahamu uchumi wa bluu na fursa zake.

Anaeleza kuwa kuna fursa nyingi ambazo Watanzania hawajazitumia inavyotakiwa katika kukuza uchumi wa bluu, licha ya kuwa kuna vyanzo vingi vilivyokidhi vigezo.

Anasema faida nyingine zitokanazo na uchumi wa bluu ni uchimbaji wa mafuta na gesi asilia baharini na pia kuwekeza kwenye nishati na manufaa mengine yanayotokana na bahari.

Mbali na hilo, anaeleza kuwa uchumi wa bluu ulianza miaka mingi iliyopita katika nchi nyingine nje ya Afrika hasa Ulaya, lakini mwaka 2016 dhana hiyo ilianza kusambaa Afrika.

Anasema mwaka jana Tanzania nayo ikaanza kuongeza nguvu katika uchumi huo, Zanzibar wakiwa ni mfano wa mchakato ulikoanzia kiasi cha kufikia hatua ya kuanzisha Wizara ya Uchumi wa Bluu na Maendeleo.

"Awali dhana ilikuwa ni kuhusu shughuli zote zinazohusiana na bahari, lakini muda ulivyosonga mbele ikawa inabadilika na mwisho hata kwenye maziwa na mito au vyazo vingine vya maji vinavyoweza kutumika katika kukuza uchumi unaotokana na maji vinaingizwa katika Uchumi wa Bluu," anasema Dk. Gurumo.



Uvuvi wa kisasa wa bahari kuu ni ajira kwa wavuvi, wasindikaji, wasafirishaji na wauza mazao ya bahari. PICHA ZOTE MTANDAO.

**HATUA ZA KUINGIA**

Dokta Gurumo anaeleza kuna hatua nne za kuingia kwenye uchumi wa bluu ambayo ni kuwa na vyanzo, mpango mkakati, utekelezaji na usimamizi.

Anabainisha kuwa baada ya kufanya hivyo, ni rahisi kuwa na mwendelezo kwa kuwa kama ni vyanzo, Tanzania ina bahari, ziwa na mito, kuhusu mikakati na utekelezaji ni suala la mamlaka kuamua kuwekeza.

Anasema usimamizi ni jambo la muhimu, kwani kama yote hayo yakifanyika bila kuwa na usimamizi matokeo yake ni kupotea kila kitu au kutopatikana faida ya kile kilichotarajiwa.

Aidha, anasema pamoja na kuwa kuna mamlaka nyingi zinazosimamia nishati mbalimbali kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji (EWURA), lakini ni muda sahihi kwa serikali kutengeneza mfumo ambao unaweza kusimamia na kuwa na kauli kuhusu uchumi wa bluu kama Zanzibar walivyofanya.

"Shughuli nyingi za uchumi wa bluu zinaingiliana na majukumu ya taasisi au mamlaka nyingine, lakini bado siyo kikwazo cha kuwa na mfumo mzuri wa kukuza uchumi wetu," anasema Dk. Gurumo.

Kwa upande wake Dk. Mumbo Mitula, mtaalamu wa masuala ya utafiti anasema: "Upya wa neno uchumi wa bluu unawachanganya wengi lakini kuna vingi wanavyovifanya vinavyohusiana japo siyo katika ubora mzuri".

Anasema; "Wanahabari mnatakiwa kuelewa dhana hii na kuwaelimisha watu wengi, pia kuwe na makongamano na mijadala mbalimbali ili wananchi wa kawaida waelewe. Wengi wanashindwa kutumia fursa zilizopo wakiwa na dhana tofauti".

Mbali na kueleza hayo, Dk. Mitula anasema: "Wapo ambao wanaona biashara inayohusiana na maji inaendana na imani za giza, zile habari za majini, mara hiki au kile zimewakatisha tamaa watu wengi. Niwaambie tu Watanzania wenzangu, kwenye biashara inayohusiana na maji kuna fursa nyingi na zikitumika vizuri zitawatoa watu wengi kwenye umasikini".

Anasema: "Wengi wanatumia maji kupata mahitaji yao machache lakini kama wakiwa na elimu nzuri kuhusu maji, wanaweza kuwekeza kwa kiwango cha juu na kupata faida kubwa. Serikali nayo ikiwekeza nguvu kwenye kuwekeza huko, miaka kadhaa baadaye uchumi utakuwa tofauti kuanzia mmoja mmoja na hata kwa taifa kwa jumla".


Katika warsha hiyo wanahabari nao walipata nafasi ya kuuliza na kutoa mchango wao kuhusiana na uchumi wa bluu, wengi walijikita zaidi kutoa maoni yao ya nini kifanyike ili dhana halisi isiendelee kuwa ngeni miongoni mwa Watanzania.



Uchimbaji wa mafuta katika pwani ya Guinea Bissau ni moja ya matunda ya uwekezaji kwenye uchumi wa bluu unaolinufaisha taifa hilo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mawaziri wetu hebu msaidieni Rais Samia






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WANANCHI kwa viongozi wao ni kama na watoto wanavyowategemea wazazi au walezi kwa kila kitu, katika ustawi wa maisha yao. Kwa hiyo wazazi na walezi wanaposhindwa kumudu kuwahudumia, huonekana hawastahili, hivyo kunyang'anywa jukumu la ulezi.

Nchi inapofanya uchaguzi, hutarajia kuona inapata viongozi ambao watabeba majukumu ya kuongoza na kuhudumia jamii kikamilifu, kulingana na mahitaji, kinyume chake wanapoteza sifa ya kuwa viongozi.

Watanzania ni watoto kwa viongozi wao. Tunafanya uchaguzi kila miaka motano kupata wabunge, madiwani na Rais na hufanya hivyo kwa matarajio ya kuwapima na kuwatathmini katika kipindi hicho na kuona kama wanatosha kuendelea.

Tumekuwa na utamaduni huo wa kupata viongozi hao kihalali na wakati mwingine kwa njia haramu ya rushwa, lakini tunakuwa nao kwa miaka yote mitano, hata kama wameshindwa kutulea, tunakwenda nao hivyo hivyo, mpaka wamalize na walipwe kiinua mgongo.

Wapo ambao wanalipwa kiinua mgongo hicho wakati mgongo haujainama. Wanakuwa hawajafanya lolote, lakini wanalipwa sawa kabisa na walioinamisha migongo kwa miaka yote hiyo, na kubaki kutung'ong'a tulioweka hapo walipo.

Kila hii miaka mitano tunachagua wabunge zaidi ya 300 na wanateuliwa mawaziri miongoni mwao, hata zaidi ya 20 na wote kwalengo la kumsaidia Rais kufanya yaliyo mema kwa wananchi ambao ndio waajiri wao wakuu.

Kwa bahati wanapokuwa wamechaguliwa au kuteuliwa katika nafasi mbalimbali, hutia matumaini makubwa kwa wananchi, kiasi cha kuwaamini, kwamba watasukuma gurudumu la maendeleo kama inavyostahili.

Wapo wanaodumu na msimamo huo wa kutumikia nafasi zao kwa kasi ile ile, lakini wapo wanaokengeuka, ama baada ya kuzoea nafasi au kwa makusudi tu, kuwa wamejisimika na kukita mizizi chini hivyo si rahisi kung'oka.

Ni sawa tu na mtumishi ambaye anaajiriwa kwenye kampuni au taasisi kwa mara ya kwanza, ambapo siku anasaini mkataba, ananyenyekea na kushangilia hata kama ni kimya kimya au kwa sauti, lakini akishazoea hubadilika na kuwa halisi na kujulikana tabia yake.

Huko nyuma, kulikuwa na semi zikihusisha waajiri asili ya Asia, ambao walikuwa wakiwatuhumu wafanyakazi wao wanaowaajiri, kwamba "Siku ya kwanza nakuja kono nyuma, lakini nazoea naweka kono bele!" Kwamba unakuja mnyenyekevu, lakini ukishazoea unajiachia na kupoteza hata nidhamu.

Tulimchagua Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Rais John Magufuli. Yeye na mwenzake wakateua mawaziri kuwasaidia kuhudumia wananchi. Wapo waliofanya vizuri lakini baadhi hawakutosha na Dk Magufuli hakusita kuwatumbua.

Dk Magufuli alipofariki dunia akamwachia Rais Samia, baadhi ya mawaziri hao, lakini naye akafanya mabadiliko madogo akateua wengine, yuko nao na tuko nao. Tunajiuliza mathalan, wa Kazi, Jenista Mhagama, anamsaidiaje Rais katika masuala ya wazee wastaafu wanaosotea mafao yao? Anamsaidiaje kuhusu kampuni na taasisi ambazo hazijawasilisha michango ya watumishi?

Wa Ardhi, William Lukuvi, anataka Rais afanye nini katika suala hili la urasimishaji makazi? Anajua nini kuhusu hii kampuni ya Land Consult inavyowafanya wakazi wa Tabata Kimanga, waliolipia Sh 300,000, lakini mpaka sasa wamekabidhiwa mawe hakuna kinachoendelea! Kwa migogoro ya ardhi kongole, lakini huku, mh!

Wa Polisi, George Simbachawene, hivi hawa madereva wa serikali walioamua kukaidi sheria za usalama barabarani na kupita kwenye njia ya mwendokasi na pia kupita barabara kuu kwa mwendo wa duma, na kusababisha ajali, Rais Samia afanye nini?

Wa Michezo, Inno Bashungwa, hivi tucheze tu soka nchini basi! Wanariadha walioipa nchi hii sifa miaka ya nyuma tunawaonaje? Tanzania yenye watu milioni 60, kweli inapeleka watu watatu Japan kwenye Olimpic, halafu tunafurahi wakirudi mikono mitupu? Rais Samia afanye nini hapa? Hivi hawa wasanii wanaoimba nyimbo za matusi na kukubaliwa kuzirekodi nazo mpaka Rais Samia afanyeje?

Mawaziri niliowataja hapa ni mahiri na wenye vipaji, lakini naona kama wanavibania. Hebu fungukeni tumsaidie Rais Samia ili kazi iendelee kwa kasi ya duma, tunataka kufika uchumi wa juu kama si leo basi kesho.

Alamsiki!

UCHUMI

## VIJANA WAIOMBA SERIKALI...

# Tunataka kuwa sehemu ya mpango huu wa maendeleo



Vijana wakijadili maeneo muhimu ya awamu ya tatu ya mpango wa maendeleo ya taifa na kuomba nafasi ya kipaumbele.**PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inaelekea kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya tatu (FYDP III), ambayo ni hatua ya mwisho ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inayojumuisha mambo yote muhimu yaliyomo katika mipango mingine ya maendeleo.

Dira ya Maendeleo' Tanzania Development Vision 2025' pamoja na mafanikio mengine imeiwezesha nchi kuingia kwenye uchumi wa kati.

Wakati taifa likielekea kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya tatu, vijana wana jambo lao kwa serikali. Wanaitaka isiwasahau iyachukue kwa uzito mawazo, vipaumbele na mahitaji yao.

Ni mapendekezo ya vijana wasomi kutoka sekta mbalimbali wakiomba serikali kuhakikisha mpango huo wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya tatu unaingiza matarajio yao kama ubunifu wao na matumizi ya sayansi na teknolojia.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam katika jukwaa la kupitia mpango huo linaloandaliwa na Asasi ya Umoja wa Mataifa ya UNA Tanzania, wanasema wana matarajio makubwa na mpango huo kutokana na ukweli kwamba vijana ni wengi, tena ndiyo nguvu kazi kubwa ya taifa na rasilimali watu muhimu iliyojikita kwenye maendeleo ya uchumi, sayansi na teknolojia.

Ofisa Miradi ya Vijana na Maendeleo wa UNA Tanzania, Lucas Kifyasi, anasema tofauti na zamani, vijana wa sasa wamebobea kwenye ubunifu na maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuongeza kuwa wengi wana eimu na ujuzi unaoweza kuchangia pakubwa katika mpango huo na hivyo kufikia malengo yake kwa haraka.

Akitolea mfano, anasema kuna vijana wengi wabunifu lakini hawana mitaji ya kuendeleza ubunifu wao ambao ungeweza kutumika kikamilifu kutatua matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii.

"Vijana wengi wamejaliwa vipaji mbalimbali kama vile ubunifu. wakiwezeshwa wakapata mitaji hata kwa riba nafuu wanaweza kutoa mchango mkubwa kwa kutumia ubunifu wao katika kutafuta majawabu ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii sasa na baadaye,' anasema Kifyas.

> **"Ndiyo maana vijana wanataka mawazo yao, vipaumbele vyao na mahitaji yao yaingizwe kwenye mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano ili utekelezaji wake uwe jumuishi,"**

"Kwa hiyo aziomba serikali, taasisi za fedha na wadau mbalimbali kutengeneza mazingira rafiki yatakayoibua ubunifu huu ili uwe msaada kwa nchi yetu," anasema.

Akitolea mfano wa janga la corona anasema Watanzania wanajifunza kuwa kama wangewekeza kwenye ubunifu ipasavyo miaka mitano iliyopita, baadhi ya changamoto kama vifaa vya kujikinga na corona vingepata ufumbuzi kutokana na ubunifu na hivyo kuipunguzia serikali gharama kubwa ya kuviagiza kutoka nje ya nchi.

"Ndiyo maana vijana wanataka mawazo yao, vipaumbele vyao na mahitaji yao yaingizwe kwenye mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano ili utekelezaji wake uwe jumuishi," anasema Kifyas.

### JUHUDI ZA KUUFAHAMU

Ofisa Mawasiliano na Uraghibishi wa UNA Tanzania, Godfrida Magubo, anawataka vijana wajitume kusoma kwa makini mpango huo na kuelewa ipasavyo hasa vipaumbele vyao ili utakapopitiwa upya na kukamilika wajivunie kuwa sehemu yake.

"Ni vizuri vijana wakasoma na kuelewa mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya tatu ikiwa ni pamoja na kuufahamu na jinsi ambavyo serikali inakusudia kuutekeleza kwa jicho la vijana," anasisitiza.

Tanzania imeingia katika uchumi wa kati jitihada zimeelekezwa zaidi katika kuendelea kujenga uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu kufikia malengo ya dira ya taifa, anasema.

Aidha, pamoja na mambo mengine sifa kuu ni kuboresha maisha ya Watanzania, kudumisha amani, usalama na umoja, utawala bora na utawala wa sheria.

Kadhalika mambo mengine ni uwepo wa jamii iliyosoma na kujenga uchumi shindani. Kutokana na hali hii, vijana wanatakiwa kuelewa mpango huo kikamilifu ili waweze kuzitambua fursa, haki zao na washirikishwe vilivyo katika michakato ya maendeleo na hivyo kufanya maamuzi sahihi.

Anasema katika mchakato huu, Wizara ya Fedha na Mipango, inatoa nafasi ya kutafuta maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwamo vijana ili kuboresha rasimu ya kwanza ya mpango huo ambapo UNA Tanzania, chini ya jukwaa endelevu la Tanzania yaani Tanzania Sustainable Platform liliitisha mkutano wa kujadii ili kupata maoni ya kuboresha mpango.

Mkutano huo unawakutanisha vijana kutoka katika sekta mbalimbali za elimu, afya, uchumi, uongozi na utawala.

Asasi ya UNA Tanzania ina imani kuwa vijana ndiyo watunga sera na watoa uamuzi wa baadaye ni kwa sababu hiyo asasi hiyo inawalenga vijana miaka yote ikiwajengea uwezo vijana zaidi ya 268,986.

Takwimu za idadi ya watu zinasema asilimia 50 ya idadi ya watu duniani wana umri wa chini ya miaka 25 na hapa Tanzania asilimia 64 wapo chini ya miaka 24 na kati yao, wenye miaka kati ya 15-35 wanafikia asilimia 34 ya idadi ya watu takribani milioni 60.

Hii ina maana kwamba vijana ni fursa na hazina ya kipekee ya taifa, wanastahili kushirikishwa katika masuala yote ya maendeleo ikiwamo mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya tatu.

Kwa upande wake Martha Luanda, kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, anasema mpango huo umeweka maeneo ya vipaumble vingi ambavyo vijana wanaweza kuvitumia kujiendeleza kiuchumi na kijamii kama viwanda, kilimo, uvuvi, ufugaji na mnyororo mzima wa thamani.

Mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano ni wa awamu ya mwisho katika utekelezaji wa dira ya maendeleo ya taifa 2025 (Tanzania Development Vision 2025) na unajumuisha mambo yote muhimu yaliyomo katika mipango mingine.



# Askofu aonya kuingiza siasa kwenye corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Makanisa ya Wabaptist Tanzania, Arnold Manase, amewaonya wanasiasa kuacha kutumia ugonjwa wa corona kufanya siasa.

Askofu Manase alitoa onyo hilo alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa kikatiba 45 wa kanisa hilo uliofanyika jijini hapa.

Alisema kuna tatizo kubwa la ugonjwa wa corona ambalo limezua mjadala mzito baina ya wataalamu, wanasiasa viongozi wa dini, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa mkanganyiko katika jamii.

"Pamoja na mambo mengine suala la kupata chanjo ni la hiari hivyo ni wajibu wa wale ambao wanajisikia amani ya moyo kuchanja wachanje na wasiyojisikia kufanya hivyo kuchanja na waache."

"Kwa kuwa suala la chanjo ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona linaendelea kujadiliwa na hakuna uhakika wa asilimia 100 basi wanaoendelea kujadili jambo hilo wasionekane wakosaji," alisema Askofu Manase.

Askofu huyo alisema kutokana na kuwapo kwa mkanganyiko huo ni vyema viongozi wa dini wakafanya maombi kwa ajili kuliponya taifa na dunia kwa ujumla na si vinginevyo.

Aliwataka wachungaji wa kanisa hilo kuendelea kuomba pamoja na waumini wao, ili taifa liwe huru kwa upande wa ugonjwa huo tishio hapa nchini.

Awali, Askofu huyo alisema kuwa kanisa hilo limekuwa likijihusisha na utoaji huduma ya elimu, maji na afya kwa lengo la kuisaidia jamii ya Watanzania.

# Waziri Mkenda aipa mwelekeo CPB

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kuhakikisha inafanya maamuzi yake kibiashara, ili kujiepusha na anguko lililozikumba taasisi zilizotangulia.

Prof. Mkenda aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua viwanda viwili cha kusaga mahindi na kuchakata alizeti vilivyopo ofisi za CPB jijini hapa.

Alisema CPB imechukua majukumu ambayo huko nyuma kulikuwa na GAPEX (kwa ajili ya kuuza mazao nje ya nchi) na National Milling Corporation (kwa ajili ya kuchakata nafaka), lakini walishindwa kuziendesha.

"Taasisi hizi zilikuwa kubwa National Milling Corporation ni taasisi kubwa sana ilianza kwa kufanya kazi kubwa sana hapa nchini baadaye ikawa mzigo na matokeo yake ikafa, na mali zilizobaki chache ndio hizo ambazo mnazo CPB, GAPEX pamoja na kuwa soko la mazao lipo ikawa mzigo na ikafutwa majukumu hayo mmepewa nyie CPB," alisema.

Alibainisha kuwa kufa kwa taasisi hizo kulitokana na kufanya maamuzi mengi kufanyika kwa misingi isiyokuwa ya kibiashara.

"Mwelekeo wenu kwa sasa ni mzuri unatupa matumaini kwamba hamtashindwa tena kama kwenye National Milling na GAPEX, naona uwekezaji unaenda, nimeona uchakataji wa korosho, naona mna kiwanda pale Dar es Salaam cha kuchataka korosho ili isiuzwe korosho ghafi," alisema Prof. Mkenda.

Alisema serikali itaisaidia bodi hiyo ifanye maamuzi yake kwa misingi ya kibiashara ili wasikumbane na anguko la taasisi zilizokufa.

Aidha, aliitaka bodi hiyo kuhakikisha wanatekeleza suala la kuingia kilimo cha alizeti cha mkataba na wakulima wakubwa na wadogo ambao watajiunga kwenye ushirika ili kusaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini.

Alisema wakifanya hivyo wao kama serikali itasimamia katika suala zima la maofisa ugani na kuzalisha mbegu bora za alizeti ambazo zitatoa mafuta kwa wingi.

Aliwataka wakulima kutumia fursa ya CPB kulima mashamba makubwa yatawawezesha kuingia kilimo cha mkataba na bodi hiyo ili kufanya kilimo chenye tija.

Akizungumzia suala la mahindi, alisema CPB wanapaswa kutangaza soko la mahindi nje ya nchi kwa sababu mahindi ya Tanzania hayana sumu kuvu.

Alisema wanapaswa kusimama imara kuhakikisha wanatangaza soko kwa sababu wamekagua mahindi na kuona yana kila aina ya sifa na ubora wa kuuzwa popote.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CPB, Dk. Anselm Moshi, alisema viwanda ambavyo wamezindua cha mahindi kina uwezo wa kusaga tani 60 kwa siku huku cha alizeti tani 40 kwa siku.

Alisema viwanda hivyo vimegharimu Sh. bilion 7.092 ambapo fedha nyingine wamepata mkopo kutoka NSSF.

"CPB imeagiza mitambo ya kisasa ya kukoboa mpunga itakayofungwa jijini Mwanza itakuwa na uwezo wa kukoboa tani 96 za mpunga kwa siku, imeshawasili na ufungaji unategemewa kuanza Agosti 21, mwaka huu na uzalishaji wake utaanza Novemba 2021," alisema.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli (kulia), akimkabidhi cheti Mkurugenzi wa Shirika la World Education Inc (WEI), Lilian Badi, ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wa shirika hilo katika kufanikisha kikao kazi cha asasi zinazotoa za elimumsingi nchini, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yatoa maelekezo utoaji vibali asasi za elimu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imeagiza utoaji wa vibali kwa asasi zinazoshughulika na masuala ya elimu msingi kwenye miradi mipya itakayoanza, uangalie utekelezaji wa afua zao kwenye halmashauri ambazo hazina wadau.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, alitoa agizo hilo alipokuwa akifunga kikao kazi cha siku tatu cha asasi 400 zinazotoa huduma katika elimu msingi.

Alisema kumekuwa na mtawanyiko usio sawa wa wadau wanaochangia ongezeko la ubora wa elimu kimkoa na halmashauri.

Naibu Katibu huyo alisema kuna halmashauri 29 hazina mdau hata mmoja licha ya uwapo wa asasi zaidi ya 400 zinazohusika na masuala ya elimu msingi.

"Kuna halmashauri sita zina wadau 15 wanaofanya vitu vinavyofanana, lakini kuna mikoa mitatu ina wadau zaidi ya 65 na mkoa mmoja una wadau 83 hili jambo haliwezi kuachwa kazi ya serikali ni kuratibu na kukaa kuwaeleza ukweli," alisema.

Alihimiza kuwapo na vikao vinavyokutanisha asasi na wadau wa elimu ili kuratibu ushirikiano kati ya serikali na wadau na vifanyike ngazi ya halmashauri na mikoa.

"Niwaagize wakurugenzi wa halmashauri na makatibu tawala wa mikoa yote kuhakikisha wana kanzidata za wadau wote wanaosaidia katika utoaji huduma kwenye elimu msingi na kuandaa vikao vya wadau angalau mara nne kwa ngazi ya halmashauri na viwili ngazi ya mikoa kila mwaka," alisema.

Mweli alisema lengo ni kufanya tathmini kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa kila mwaka.

Aliitaka mikoa kuhakikisha inawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maelekezo hayo kila robo ya mwaka na ofisi ya TAMISEMI itakuwa na vikao mara mbili kwa kipindi hicho.

Aidha, alitoa rai kwa asasi za kiraia zinazoshughulika na sekta hiyo kuendelea kuungana na serikali katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Alisema wafadhili wanapaswa kutoa ajenda, lakini asasi ziandae mradi.

"Kama wafadhili ndio wanaoandaa mradi tunafanya makosa, wao wanapaswa kuandaa ajenda nyie mwandae mradi muwapelekee wautathmini na watoe fedha, muandae mradi wa kumsaidia mtoto wa kitanzania, msiwe wanaharakati mkikutana na wafadhili muwaambie ukweli," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Asasi za Kiraia, Lilian Badi, aliishukuru serikali kwa kuandaa kikao kazi hicho, ambacho kimefanikiwa kuwaunganisha watoa huduma hizo na viongozi wa serikali.

Badi alisema ni jukumu la asasi hizo kupeleka huduma kwenye maeneo yote nchini ili kutoa usawa wa huduma kwa wananchi.





# Ma-DC wa Tanzania na Malawi waweka mikakati

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

KATIKA kuhakikisha diplomasia na kukuza uchumi baina nchi za Tanzania na Malawi inaimarika wakuu wa Wilaya ya Ileje na Chitipa wamekutana ili kuweka mikakati ya utekelezaji ili kufikia malengo ya kujenga mahusiano baina ya nchi zote mbili.

Mikakati ya kukuza diplomasia na uchumi baina ya nchi ya Tanzania na Malawi imefanyika juzi katika Mji wa Chitipa ulioko nchini Malawi huku ikihusisha viongozi pamoja na wataalamu.

Katika kikao hicho Mkuu wa Wilaya ya Ileje iliyoko mkoani Songwe, Anna Gidarya, aliomba uongozi wa Wilaya ya Chitipa kushughulikia vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha shughuli za uzalishaji mali.

Alisisitiza kuendelea kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao na kufungua fursa za masoko katika mji wa Ileje na Chitipa ili kukuza uchumi pamoja na kulipa kodi kwenye mamlaka zinazohusika.

"Pamoja na mambo mengine tumeweza kujadili masuala ya amani ambayo ni msingi mmojawapo wa nyenzo ya kukuza uchumi, tumejadili namna ya kuzuia maambukizi ya COVID-19 pamoja na magonjwa ya mazao na mifugo katika mpaka wa Isongole ambao unazidi kuimarika kutokana na uwapo wa barabara ya lami toka Mpemba hadi Isongole upande wa Tanzania," alisema Gidarya.

Vile vile, alisema kikao hicho kimeridhia kuhusu kuwa na mpango wa pamoja wa kukabiliana na wahalifu wanaotumia mpaka kujificha upande mmojawapo wa nchi hizo ikiwamo biashara za magendo.

Mkuu wa Wilaya ya Chitipa, Stuart Ngoka, aliipongeza Tanzania kwa kuandaa kikao cha pamoja kwa lengo la kujadili vikwazo na kutatua kwa pamoja ili kuinua uchumi wa wananchi.

Alisema wanatarajia kufanya ziara wilayani Ileje siku zijazo pamoja na kukagua na kujifunza miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa.

Tanzania na Malawi zina uhusiano wa wakuu wa nchi, mabalozi pamoja na michezo ambayo pia katika kikao cha jana imesisitizwa.



Wananchi wa Kata ya Hasanga, mkoani Songwe, wakishiriki katika ujenzi wa kituo cha afya, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mil. 44/- zatumika ujenzi vyumba vya madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

JUMLA ya Sh. milioni 43.8 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu katika Shule ya Sekondari Wasichana Kayuki iliyopo Kata ya Ilima, wilayani Rungwe.

Fedha hizo zimetokana na michango ya wananchi wanaozunguka shule hiyo pamoja na serikali ambazo zilitolewa katika vipindi tofauti ili kukamilisha ujenzi wa madarasa na ofisi za walimu shuleni hapo.

Akizungumza jana mbele ya kamati ya siasa ya Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kayuki, Mwalimu Betha Sarufu, alisema kukamilika kwa vyumba hivyo kutasaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi darasani na watasoma kwa utulivu.

Alisema baada ya kukamilika kwa vyumba hivyo kutaweka uwiano sawa kati ya idadi ya wanafunzi na mwalimu katika darasa na itachochea ufaulu wa masomo kwa kuwa watasoma kwenye mazingira mazuri.

"Nawashukuru sana wananchi wa Kata ya Ilima kwa kuendelea kutoa michango ya nguvu kazi na fedha ili kujenga vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu mmewasaidia watoto wetu kusoma kwenye mazingira mazuri nawaomba msichoke bado tunahitaji msaada wetu maana keki ya taifa ni ndogo kila eneo wanaihitaji," alisema Mwalimu Sarufu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, pamoja na kamati ya siasa walifurahishwa na uchapakazi wa mwalimu huyo na kuiomba Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya kumpandisha cheo Sarufu baada ya kuridhishwa na takwimu za ufaulu, nidhamu ya wanafunzi, usimamizi wa miradi ya ujenzi pamoja na mazingira nadhifu ya shule hiyo.

Katika hatua nyingine, serikali imetoa Sh. bilioni 2.77 kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 7.2 ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Kata ya Mpuguso hadi Kisondela.

# Mbunge Mwakagenda ataka wananchi kujilinda na corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, amewaomba wananchi kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya kuhusu kujikinga na ugonjwa wa corona pamoja na kupata chanjo ya ugonjwa huo.

Mwakagenda alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe kwa kuwataka wananchi wapuuze kauli za upotoshaji zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa kuhusu chanjo ya corona na kuwaomba kuendelea kupata chanjo hiyo ili kukabiliana na ugonjwa huo ambao umekuwa tishio kwa sasa.

"Tufuate ushauri na maelekezo ya wataalamu wetu wanavyotaka sisi wanasiasa tuna mambo yetu, suala la afya halihitaji mzaha lazima tuzingatie sayansi wanahamasisha wananchi wote wapate chanjo ili kukabiliana na adui huyu ambaye anagharimu maisha ya jamaa na ndugu zetu," alisema Mwakagenda.

Vile vile, aliwataka wananchi kuwa makini na kauli zinazotolewa na viongozi wa kisiasa na wakiendelea kumtegemea Mungu ili kujiepusha na janga hilo la corona.

Hivi karibuni kumekuwa na mvutano wa baadhi ya kauli ya viongozi kuhusiana na chanjo ya corona huku kila mmoja akitoa maoni yake na kuwaacha njia panda wananchi licha ya serikali kupitia Wizara ya Afya kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo hiyo.

Rais Samia Suluhu Hassan wakati akizundua chanjo hiyo alisema ni salama na wananchi wanapaswa kuchanjwa ili kukabiliana na ugonjwa huo. Alisema jopo la wataalamu wa afya lilitafiti na kujiridhisha kwamba chanjo hiyo ni salama kwa matumizi ya wananchi.

Aliwaomba Watanzania kuachana na upotoshaji ambao wakati mwingine unatokana na vita ya kibiashara na waendelee kujilinda dhidi ya ugonjwa huo hatari.



## Rais Samia kuzindua tamasha la Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAMASHA la Kizimkazi linatarajiwa kuanza Agost 23, mwaka huu na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa tamasha hilo kwa mwaka huu.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya tamasha hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, alisema Rais Samia ataambatana na viongozi mbalimbali na katika uzinduzi huo, kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo usafi wa mazingira, mafunzo na maonyesho ya wajasiriamali 300.

Alisema tamasha hilo lilianza rasmi mwaka 2016 kwa jina la Samia Day, wakati huo akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwataka Wanakizimkazi kukutana kila mwaka ili kutafakari maendeleo yaliyopatikana na changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi na kuleta maendeleo.

Pia, alisema kwa mwaka huu tamasha hilo limedhaminiwa na Benki ya CRDB na kuipongeza benki hiyo ambayo imekuwa ikifanya shughuli zake mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa ukumbi wa mitihani na madrasa Shule ya Sekondari Kizimkazi, Nyumba ya Maendeleo ya Shehia.

"Nisiwe mkosefu wa fadhila kwa upekee nawashukuru waliotangulia kuchangia maendeleo ya tamasha hili kwa nyakati mbalimbali wakiwamo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Benki ya NMB na NBC na watu binafsi," alisema.

Alisema kuwa katika tamasha hilo, kumeandaliwa utaratibu wa wananchi kupata chanjo ya corona kwa anayetaka.

Naye, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa, alisema kupitia sera ya uwekezaji kwenye jamii waliona ni vyema kuwa ni sehemu ya wadhamini wa tamasha hilo.

Alisema lengo la CRDB ni kulifanya tamasha hilo kuwa endelevu, lenye kutangaza vivutio mbalimbali vya Zanzibar, kuchochea utunzaji wa mazingira na kutoa fursa za kiuchumi kwa wana Kizimkazi kijiji ambacho anatokea Rais Samia.

"Kizimkazi ina utajiri mkubwa wa vivutio vya kiutalii ikiwamo fukwe, samaki aina ya dolphins, hoteli za kisasa, tamaduni na historia ya Kizimkazi, kupitia matangazo yetu mbalimbali mtaona na kusikia hazina kubwa iliyoko Kizimkazi," alisema.Alisema, dhamira ni kuboresha maisha ya jamii na kufanya kilicho bora wakati wote na kuboresha Kizimkazi Day ili kuleta tija kwa wana Kizimkazi na Zanzibar kwa ujumla na waliona ni vyema kuboresha tamasha hilo kutoka Kizimkazi Day na kuwa Kizimkazi Festival.

# Abdulla atoa siku 10 kuangamiza bidhaa zilizopita muda wake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa muda wa siku 10 kuangamiza au kurejesha zilipotoka bidhaa zilizopitwa na wakati.

Hemed alitoa agizo hilo wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika Bandari ya Malindi Jijini Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais alitembelea ghala lililohifadhiwa mafuta lainishi ambayo yaliingizwa nchini mwaka 2019 kutoka Dubai na kukosa kiwango kwa matumizi ya vyombo vya usafiri.

Alisema ni vyema wizara ikahakikisha Zanzibar haipokei bidhaa zilizopitwa na wakati kwa usalama wa wananchi wake, pamoja na kuitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuchukua hatua kali kwa wafanyabiashara wanaoingiza bidha zilizopitwa na wakati ili iwe fundisho kwa wafanyabiashara wengine.

"Zanzibar sio sehemu ya kuja kutupa bidhaa zisizo salama, naitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha inachukua hatua kali kwa wahusika wanaoleta bidhaa hizo kwa kufuata sheria na taratibu," alisema.

Katika ziara hiyo Hemed alikagua mchele aina ya Asha Kuku, ulioletwa na kampuni ya A.R.Y ulioingia Zanzibar Julai 11, mwaka huu na mchele ulioletwa na I.A Siwje Traders ulioingia Juni 30, mwaka huu, ukiwa ni jumla ya kontena 10 sawa na tani 260.

Aliitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), kumaliza kesi ya mchele wa I.A Siwji Trader na kampuni hiyo imeashiria kutenda vitendo vya uhujumu uchumi kwa kutoa rushwa ili kuhalalisha bidhaa yake iliyokwishapitwa na muda.

Akitoa taarifa kuhusu bidhaa ya mafuta lainishi, Kaimu Mkurugenzi Mamlaka ya Viwango Zanzibar (ZBS), Muhamed Mwalim Simai, alisema bidhaa hiyo ilikaguliwa na TBS na kukataliwa na hatimaye mhusika huyo kuhamishia Zanzibar bidhaa hiyo na ZBS imeizuiia kuingia sokoni.

Kwa upande wake Mkuu wa usajili na tathmini ya chakula kutoka Taasisi ya Udhibiti wa Dawa na Chakula (ZFDA), Khadija Ali Sheha, alisema mchele ulioingizwa Zanzibar kutoka kampuni hizo umeshafanyiwa vipimo na kuonekana kupitwa na wakati na kugundulika kuwa haufai kwa matumizi ya binadamu na mamlaka yao imetoa maelekezo kwa wahusiku kuchukua hatua zaidi.

Wakati huo huo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alitembelea gati kuu ya Malindi na kutoridhishwa na mandhari ya eneo hilo kutokana na uchakavu wa miundombinu.

Katika kulipatia ufumbuzi tatizo hilo la miundombinu Makamu wa Pili amempa muda wa wiki moja Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari kuhakikisha maeneo yote yalio na hitilafu kwa usalama wa wananchi yanafanyiwa marekebisho.

"Naomba mfahamu kuwa Bandari hii ndio uso wa Zanzibar yetu haifurahishi bandari yetu kuwa katika mandhari kama hii isiyoridhisha," alisema Hemed.

Pia alikagua eneo la kupumzikia abiria, Ofisi ya Uhamiaji, ofisi ya wakaguzi wa afya na kutoridhishwa na mazingira ya maeneo hayo.




Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu tamasha la Kizimkazi, linalotarajiwa kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Agosti 23, mwaka huu. Kulia ni Mkuu wa mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jaji Mkuu ataka haki za binadamu kuzingatiwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, amesema masuala ya haki za binadamu ni kati ya vitu vya msingi sana kutokana na kugusia stahiki ambazo zinampasa kuzifaidi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua warsha ya mawakili na wanasheria Zanzibar ambayo imeandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za binadamu Tanzania (THRDC), mjini hapa.

Alisema kuwanyima watu haki zao ni sawa na kuukanusha ubinadamu wao na hakuna haki zenye uzito ambazo anapaswa kuwa nazo, zaidi ya haki hiyo.

Alisema matumaini yake mkusanyiko huu pamoja na mambo mengine utajadili namna ambavyo mawakili wanapaswa kuendesha kesi zenye maslahi kwa umma, haki za binadamu, uhuru wa kujieleza kwa viwango vya kitaifa na vile vya kimataifa.

Alisema katika mafunzo hayo mawakili hao watajifunza ufunguzi wa mashauri ya kimkakati na mambo mengine yenye mnasaba na utekelezaji wa haki za binadamu.

Aliwaomba washiriki hao kuwa makini katika mafunzo hayo kwa vile, masuala yaliyopangwa kujadiliwa yanagusa msingi na heshima ya ubinadamu.

"Haki za binadamu ni kati ya vitu vya msingi sana kwa vile yanagusia stahiki ambazo zinampasa kila binadamu kuzifaidi kwa kuwa yeye ni binadamu. Haki hizi kwa lugha nyingine huitwa ni haki ambazo binadamu huzaliwa nazo," alisema Makungu.

Naye Mratibu wa mtandao wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema mawakili hao watapata uzoefu na kuwasaidia wananchi wanapohitaji kusaidiwa kuendesha mashauri ya haki za kibinadamu na kikatiba.

Alisema wananchi wanapaswa kutumia njia za busara kudai haki kwa kwenda mahakamani na sio kwenda barabarani kufanya vurugu.

"Mawakili na wananchi wakielewa vizuri kudai haki zao kupitia mahakama kutapunguza malalamiko na uonevu," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud, alisema mafunzo hayo ni ya kipekee ambayo yatawasaidia mawakili hao kutetea haki za binadamu.

Alisema kuwa kwa muda mrefu kuna utetezi, lakini mawakili wanafanya kazi zao bila kuwa na mifumo na mipango mikakati ya kutetea wanapokuwa mahakamani.

"Mafunzo haya yataongeza uelewa na watakaposimama mahakamani wawe wanafanya utetezi kwa kujiamini na kufuata misingi na taratibu za sheria," alisema.

Alisema hivi sasa kuna mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia hata watenda makosa wanambinu nyingi hivyo bila kuwa na mafunzo ya mara kwa mara kunasaidia kutuweka pamoja na kujua mbinu za watendaji makossa," alisema Jamila.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AKI AKI KIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SCANIA** yenye namba za usajili **T 148 DTP** engine namba **6622523,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **MKB/TR/RB/150/2021**

116415802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AUGUSTINE LUHWANO KISINGA** anatangaza kupotelewa na kadi yagari aina ya **NISSAN PATROL** yenye namba za usajili **T 314 DTQ,** chasis namba **ZD39205588**,engine namba **JNITESY6140143826,** yeyota atakayeiokota atoe taarifa kituo chochte cha polisi

Polisi taarifa

**MKB/TR/ RB/150/2021**

116415702

## KUPOTEA KWA CHETI

**INDEPENDENCE POWER TANZANIA LIMITED (IPTL)** wanatangaza kupotelewa na cheti cha kampuni chenye namba za usajili **121713** kilichotolewa na **BRELA 20th** mwezi wa **2 mwaka 1997**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**DAR/CEN/ RB/396547/2021**

116415202

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN SOSPETER** anatangaza kupotelewa na cheti cha **AC13003119C** chenye index namba **S2354-0604** kilichotolewa na shule ya secondary **EAGLES** mwaka **2013**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DAR/URA/ RB/406187/2021**

116415502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **ODILO KAPIS TWEVE** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki yenye usajili Namba. **MC 959 BBL** Chasis Namba. **LBRSPJB58E9011457** Engine Namba.14921109 Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Rb Namba.MOR/MOR/ RB/855055/2020.**

116415402

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**RAMADHANI HAMISI JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili **MC 632 CJJ** aina ya **TVS KING.** Chasisi namba **MD6M14PA6K4G08763,** Engine namba **AK4GK4X08821** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**MAN/BAB/RB/319692/2021**

116415602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZNIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NO 115 YA 2021**
**HERIOLOTU BONIFACE SITAYO……MDAI**
**DHIDI YA**
**ALLY HEMED NASSORO……1.MDAIWA**
**SALUM SULTAN KHALFAN……..2.MDAIWA**
**AHMED ALLY HEMED……..3.MDAIWA**
**Kwa,**
**1.ALLY HEMED NASSORO**
**2.SALUM SULTAN KHALFAN**
**3.AHMED ALLY HEMED**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelelzo ya madai yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii,kwa hiyo unahitajika mahakama hii binafsi,wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **jumatatu 13 mwezi 09 mwaka 2021 saa 2:30 asububhi**

Kwa mujibu wa madai hayo ,na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinanzohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

**ANGALIZO.**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitika kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindqa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo **tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2021**

116416502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **ALLY HUSSEIN SAID** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 477 BHL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi:

**TAN/RB/404491/2021**

116417002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA 63)**
**Mahakama ya Mwanzo Nyabiyonza**
**Wilaya ya Karagwe**
**MADAI YA TALAKA NO. 2/ 2021**
**Mdai …………..Meshack Marco**
**Mdaiwa ………Advelina Chungu**
**Kwa Advelina Chungu**

Kwa kuwa mdai ameleta madai ya talaka kwamba anataka kuvunja ndoa yake na mdaiwa, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Jumatano tarehe 01/09/2021 saa 2:00 Asubuhi. Kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Huu wito umetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 10/08/2021**

RESIDENT MAGISTRATE NYABIYONZA P. COURT KARAGWE

116417102

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu Samson Thomas Kidicha** wa Bukoba, anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC756 APB**, Injini na. **OF5D91542035** na Chessis na. **MD625GF5891D09465.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/406709/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0766225839**

116417202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**………..MJINI TANGA**
**Usimamizi wa**
**Mirathi…………….115…………2021**
**Ombi la……JOHN SAIDI**
**EDWARD……..Kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**…..EDWARD THOMAS SAIDI….**
**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 31/8/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 10/8/2021**

116417302

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Hichilema aja na sera mpya ya kiuchumi

**Lusaka, ZAMBIA**

RAIS mteule wa Zambia Hakainde Hichilema, amesema anapanga kuzindua sera kadhaa za kufufua uchumi, kwenye taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa madini, mara baada ya kuingia ofisini, wiki ijayo.

Hichilema ambaye ni mmoja wa wafanyabiashara wakuu Zambia na pia kiongozi wa chama kikuu cha upinzani cha UPND, ameyasema hayo juzi, mbele ya wanahabari, nyumbani kwake kwenye kitongoji cha Kanyama, mjini Lusaka.

Hichilema ambaye amewania urais mara sita, Jumatatu wiki hii, alitangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais na kufikisha kikomo utawala wa miaka sita wa rais Edgar Lungu.

Kiongozi huyo alipata jumla ya kura milioni 2.8 dhidi ya milioni 1.8 alizopata Lungu, ikiwa ni ushindi wa zaidi ya asilimia 50 iliyohitajika, ili kutangazwa mshindi.

Lungu alikubali matokeo hayo wakati akiapa kuhakikisha ubadilishanaji madaraka wenye amani.

Hata hivyo hapo awali, muda mfupi baada ya uchaguzi kufanyika, Lungu alidai kuwa haukuwa wa haki na ukweli.

**VOA**



Wakazi wa mji wa Les Cayes nchini Haiti, jana wakiwa wamelala nje ya makazi yao ambayo yaliharibiwa kutokana na tetemeko la ardhi, lililotokea mwishoni mwa wiki lenye ukubwa wa 7.2 kipimo cha Richter **PICHA: REUTERS**

## Kenya yarejesha raia wake kutoka Afghanistan

**Nairobi, KENYA**

KENYA imesema kuwa iko kwenye mchakato wa kuwaondoa Wakenya wote, waliokwama Afghanistan, kufuatia hatua ya Taliban kudhibiti Kabul.

Katika taarifa, Wizara ya Mambo ya Nje imesema kuna Wakenya 12 ambao walikuwa wanafanyakazi katika taasisi tatu tofauti, tayari wameondolewa huko.

Serikali iliwasiliana na taasisi husika na kuomba hatua za haraka zifanyike, huku watatu tayari wameondolewa nchini humo ilhali tisa wangali hawajasafirishwa.

Kenya haina ubalozi au ofisi za diplomasia nchini Afghanistan na kufanikisha hilo, inabidi kutumia ubalozi wa Kenya wa Islamabad, Pakistan, pamoja na kuwatumia wanadiplomasia wa kigeni.

**BBC**

## Raia 47 Burkina Faso wauawa katika shambulio

**Sahel, BURKINA FASO**

TAKRIBANI raia 30 pamoja na askari 14 wameuawa katika shambulio la msafara kati ya eneo la mji wa Dori na Arbinda nchini Burkina Faso.

Watu ambao walikuwa wakiondoka katika mji wa Dori kuelekea mji wa Arbinda kwenye umbali wa kilomita 100 wamelengwa na shambulio hilo jipya.

Vikosi vya ulinzi na raia wanaojitolea kwa ulinzi wa taifa, walifanikiwa kuangamiza magaidi 58 kulingana na chanzo cha usalama.

Rais Roch Marc Christian Kaboré alitangaza maombolezo ya kitaifa ya saa 72 kuanzia jana.

Kutokana na hali ya ukosefu wa usalama katika Mkoa wa Sahel, raia wanaotaka kufanya safari kati ya miji miwili ya Arbinda na Dori, karibu kilomita 100, hawatumii barabara peke yao, wanasindikizwa na vikosi vya usalama.

Wafanyabiashara ambao walikuwa wamesindikizwa na askari kutoka Dori kwenda Arbinda, walijikuta wakishambuliwa na watu wenye silaha.

Askari na raia wanaojitolea kwa ulinzi wa taifa walikuwa wakilinda usalama wa raia hao, kulingana na chanzo rasmi.

Shambulio hilo lilitokea katika kijiji cha Boukouma kilomita 25 kutoka eneo la Gorgadji.

Raia 30 waliuawa na wanajeshi 14 na raia wanaojitolea watatu kwa ulinzi wa taifa, pia waliuawa katika shambulio hilo, kulingana na duru rasmi.

**RFI**

## Rais Afghanistan adai alikimbia akihofia kunyongwa akihutubia

**Abu Dhabi, U.A.E**

KWA mara ya kwanza tangu mji mkuu wa Afghanistan, Kabul, kuangukia mikononi mwa Taliban, rais aliyetimuliwa mamlakani Ashraf Ghani alizungumza, jana, Agosti 18, kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E), alikopata hifadhi ya ukimbizi.

Amesema ilibidi akikimbilie katika Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E) kwa sababu walitaka kumnyonga hadharani.

Katika hotuba yake kwa taifa, rais aliyeondolewa mamlakani amekiri kushindwa kisiasa na kijeshi dhidi ya Taliban, ambao wameanzisha mazungumzo na viongozi wa zamani wa Afghanistan.

Rais wa zamani Hamid Karzai alikutana kwa ajili ya mazungumzo na kiongozi kutoka kundi hilo, Anas Haqqani.

Ashraf Ghani alionekana peke yake mbele ya kamera, akiwa amevaa shati jeupe na koti jeusi, bendera ya Afghanistan ikiwa nyuma yake, ameripoti Vincent Souriau mwandisi RFI Dubai.

"Ilibidi nikimbilie katika Umoja wa Falme za Kiarabu kwa sababu walitaka kuninyonga hadharani," amebainisha Ashraf Ghani.

Mapema jana, serikali ya U.A.E ilitangaza kuwa iko tayari kuwapokea kwa sababu za kibinadamu rais huyo wa zamani na familia yake.

"Kushindwa huku ni kwetu na kwa washirika wetu wa kimataifa."

Ashraf Ghani anadai: "Niliondoka nchini kwa kuzuia damu nyingi zisimwagike na uharibifu wa mji wa Kabul".

"Ndio, ni tumeshindwa, lakini tumeshindwa sote, serikali yetu na washirika wetu wa kimataifa, sote tumeshindwa dhidi ya vita vya Taliban. Kwa sababu kile kilichoanza kama mchakato wa amani kimemalizika kama vita," amebainisha rais Ashraf Ghani.

"Sasa lazima tujadili, na ninaunga mkono mazungumzo yaliyoanzishwa na Taliban na rais wa zamani Hamid Karzai. Lakini mimi, sintochoka. Ninajadili jinsi ya kurudi nyumbani Afghanistan, ambapo nitaendelea kupigania haki na maadili yetu, "aliongeza rais Ghani.

Lakini, wakati Taliban wamerudi madarakani, ushawishi wa Ghani umeshuka. Siku ya Jumatano wiki hii, Marekani ilibaini kwamba rais huyo wa zamani sio mtu tena wa kutegemea nchini Afghanistan.

***RFI***

## Vikosi vya Marekani kuwasaka waasi msituni DRC

**Kinshasa, DRC**

VIKOSI maalum vya Operesheni kutoka Marekani vimewasili Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kusaidia kukabiliana na wapiganaji wa Jihad waliojificha katika msitu wa eneo hilo.

Ofisi ya Rais Felix Tshisekedi, ilisema hayo mwishoni mwa wiki, kwamba Kinshasa iliomba wanajeshi hao kupelekwa katika eneo hilo, ili kulisaidia jeshi la DRC, dhidi ya waasi wa ADF.

Idadi ya wanajeshi hao kufikia sasa haijulikani, wanajeshi wengi wameonekana katika picha rasmi kati ya Tshisekedi na ujumbe ulioongozwa na balozi wa Marekani nchini DRC Mike Hammer.

DRC na Marekani zilikithibitishia chombo cha habari cha AFP, kuhusu uwapo wa baadhi ya wanajeshi hao katika kambi moja katika mbuga ya Wanyamapori ya Virunga, wanakoishi sokwe walio katika hatari ya kuangamia.

Rais Tshisekedi alisema kwamba wanajeshi hao watawasaidia maofisa wa kuwalinda wanyamapori katika Mbuga ya Garamba, ambayo sawa na Virunga imekuwa eneo ambalo vikosi hivyo vya waasi vimekuwa vikiishi.

Operesheni hiyo inatarajiwa kufanya kazi kwa majuma kadhaa' na watawalenga wapiganaji wa ADF, taarifa yao imeeleza kuwa tawi la Daech au wanamgambo wa Islamic State.

***BBC***

MECHI KALI
HOME
AWAY
BREST
9.01 | 5.77 | 1.28
PARIS ST GERMAIN

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 433

# KANE HATIHATI KUIVAA WOLVES JUMAPILI



**LONDON, England**

NUNO Espirito Santo hana uhakika kama mshambuliaji wake, Harry Kane ataichezea Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya timu ya zamani ya kocha huyo, Wolves, hapo Jumapili.

Spurs ilisafiri Jumatano kwenda nchini Ureno kwa ajili ya mchezo wa kufuzu kucheza michuano ya Europa Conference dhidi ya Pacos de Ferreira.

Kane, ambaye bado anaripotiwa anataka kuondoka klabuni hapo kujiunga na Manchester City, hakujumuishwa kwenye safari ya kikosi hicho, ingawa Spurs wamedai nahodha huyo wa England bado anajifua, kwa ajili ya kujiweka fiti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye alirudi kujiunga na mazoezi ya timu yake hiyo Ijumaa, hakucheza wakati Spurs wakiifunga City, Jumapili.

Wolves, timu ambayo Nuno aliondoka msimu uliopita, ndio watakaocheza na Tottenham kwenye mchezo unaofuata wa Ligi Kuu England, ingawa uwezekano wa Kane kuwapo bado haujulikani.

"Siwezi kujibu swali hili. Naweza kujibu kwamba, anaendelea vizuri na atajiunga na kikosi kesho (leo) Ijumaa. Halafu tutaona," alisema Nuno akiwaambia waandishi wa habari.

"Yupo bora zaidi kuliko jana na matumaini yetu atakuwa bora zaidi kesho. Na wachezaji wote kwa sasa wanajifua, ili kuwa fiti."


Alipoulizwa kama amewasiliana na Kane, Nuno alisema: "Tunazungumza na wachezaji wote kila siku. Ni kawaida kwamba tunazungumza na wote."

# Llorente kuzeekea Atletico Madrid

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Atletico Madrid, Marcos Llorente amesaini mkataba mpya kuendelea kubakia kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, hadi mwaka 2027.

Mkataba wa sasa wa kiungo huyo ulikuwa unamalizika mwaka 2024, lakini Atletico wamethibitisha jana kuwa nyota huyo amesaini mkataba mwingine wa miaka mitatu.



Llorente anakumbukwa kwa mabao yake mawili dhidi ya bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool Machi 2020, lakini amekuwa mchezaji muhimu kwa kikosi cha Diego Simeone tangu alipojiunga hapo akitokea kwa majira zao Real Madrid kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 40 mwaka 2019.

Alifunga mabao 12 na asisti 11 wakati Atletico wakitwaa taji lao la kwanza la LaLiga tangu msimu wa 2013-14, na likiwa la tatu tangu mwaka 1996.

Ni Jose Luis Morales pekee aliyefunga mabao mengi (13) kuliko mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kati ya viungo wote msimu huo, huku asisti zake 11 zikiwa nyingi zaidi kwa nafasi mchezaji kiungo kwenye LaLiga, akihusika pia na mabao 23.

Licha ya uvumi wa muda mrefu kumhusisha na Manchester United au Paris Saint-Germain, kusaini kwa mkataba huo mpya kunamfanya Llorente sasa kuzima kelele hizo, wakati Simeone akipambana kukiimarisha kikosi chake.

Atletico walianza mchezo wao wa kwanza wa kutetea taji la LaLiga kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Celta Vigo.

HABARI MICHEZO


3,401,140

# JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/08/21 | 17:00 | Crystal Palace vs Brentford | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 02. 21/08/21 | 17:00 | Leeds vs Everton | 2.22 | 3.53 | 3.12 |
| 03. 21/08/21 | 17:00 | Coventry vs Reading | 2.20 | 3.25 | 3.20 |
| 04. 21/08/21 | 17:00 | Cardiff vs Millwall | 2.24 | 3.21 | 3.16 |
| 05. 21/08/21 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 06. 21/08/21 | 18:00 | Alaves vs Mallorca | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 07. 21/08/21 | 19:30 | Verona vs Sassuolo | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 21/08/21 | 20:30 | Granada vs Valencia | 2.49 | 3.28 | 2.87 |
| 09. 22/08/21 | 16:00 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.42 | 3.22 | 2.21 |
| 10. 22/08/21 | 16:00 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.40 | 3.36 | 2.77 |
| 11. 22/08/21 | 16:00 | Bordeaux vs Angers | 2.80 | 3.30 | 2.48 |
| 12. 22/08/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Malaga | 2.73 | 2.78 | 2.87 |
| 13. 22/08/21 | 21:45 | Nice vs Marseille | 2.88 | 3.18 | 2.48 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 20 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3185 | Daegu vs Gwangju | 1.89 | 3.25 | 3.88 |
| 14:45 | 2423 | Hougang United vs Geylang Int. | 1.53 | 4.26 | 4.84 |
| 16:00 | 2217 | FC Elva vs Parnu Jalgpalliklubi | 2.63 | 4.17 | 2.22 |
| 18:00 | 1215 | Slutsk vs Vitebsk | 2.52 | 3.10 | 2.66 |
| 18:00 | 3945 | Znojmo vs Blansko | 3.47 | 4.05 | 1.78 |
| 18:00 | 5867 | Mamelodi Sundowns vs Amazulu | 1.54 | 3.68 | 6.28 |
| 18:30 | 5797 | Haka vs AC Oulu | 2.01 | 3.15 | 3.59 |
| 19:00 | 4679 | Jihlava vs Graffin Vlasim | 2.24 | 3.43 | 2.80 |
| 19:30 | 1870 | Hannover vs Heidenheim | 2.29 | 3.32 | 2.97 |
| 19:30 | 5010 | Fortuna Dusseldorf vs Holstein Kiel | 2.00 | 3.50 | 3.45 |
| 19:30 | 5608 | Vorskla Poltava vs FC Metalist 1925 | 1.59 | 3.72 | 5.02 |
| 19:55 | 4095 | Mladost Lucan vs Radnik Surduluca | 2.28 | 3.19 | 2.90 |
| 20:00 | 1007 | Hlucin vs Vratimov | 1.74 | 4.45 | 3.38 |
| 20:00 | 1261 | Esbjerg vs Hvidovre IF | 2.75 | 3.42 | 2.28 |
| 20:00 | 3980 | Ismaily SC vs Wadi Degla | 1.96 | 3.25 | 3.89 |
| 20:00 | 4610 | Midtjylland vs Silkeborg | 1.45 | 4.53 | 6.11 |
| 20:00 | 4660 | Enppi Club vs Talaea El Gaish | 2.56 | 3.10 | 2.76 |
| 20:30 | 1271 | Kayserispor vs Adana Demirspor | 2.91 | 3.11 | 2.44 |
| 20:30 | 2374 | Samsunspor vs Balikesirspor | 1.18 | 5.99 | 12.56 |
| 21:00 | 1392 | Valladolid vs Zaragoza | 1.72 | 3.25 | 5.32 |
| 21:00 | 2555 | Maastricht vs Helmond Sport | 2.60 | 3.53 | 2.40 |
| 21:00 | 3749 | FC Arouca vs Famalicao | 3.05 | 2.96 | 2.44 |
| 21:00 | 3920 | Den Bosch vs Jong Ajax | 2.43 | 3.81 | 2.43 |
| 21:00 | 4136 | ADO Den Haag vs Emmen | 2.83 | 3.66 | 2.18 |
| 21:00 | 4501 | Dordrecht vs Jong Utrecht | 2.84 | 3.52 | 2.23 |
| 21:00 | 4960 | Zlate Moravce vs FK Pohronie | 2.27 | 3.40 | 2.77 |
| 21:00 | 5221 | Hrvatski Dragovoljac vs Hajduk Split | 8.87 | 5.60 | 1.24 |
| 21:00 | 5394 | Telstar vs Roda Kerkrade | 3.07 | 3.66 | 2.06 |
| 21:00 | 5936 | NEC Nijmegen vs PEC Zwolle | 2.51 | 3.20 | 2.75 |
| 21:00 | 5941 | SBV Excelsior vs FC Volendam | 2.83 | 3.91 | 2.10 |
| 21:00 | 5991 | De Graafschap vs NAC Breda | 1.94 | 3.67 | 3.38 |
| 21:30 | 1943 | RB Leipzig vs Stuttgart | 1.46 | 4.78 | 5.78 |
| 21:30 | 2033 | Farul Constanta vs Dinamo Bucuresti | 1.46 | 4.14 | 6.51 |
| 21:30 | 3609 | FC Winterthur vs FC Thun | 2.72 | 3.20 | 2.41 |
| 21:30 | 3618 | Radomiak Radom vs Warta Poznan | 1.98 | 3.29 | 3.48 |
| 21:30 | 5986 | Frosinone vs Parma | 3.06 | 3.11 | 2.35 |
| 21:45 | 1356 | Standard Liege vs Oostende | 2.12 | 3.35 | 3.30 |
| 21:45 | 1601 | Athlone Town vs Galway United | 3.87 | 3.96 | 1.71 |
| 21:45 | 1948 | Dundalk FC vs Drogheda Utd | 1.60 | 3.95 | 5.60 |
| 21:45 | 2742 | Bristol City vs Swansea | 2.42 | 3.05 | 3.00 |
| 21:45 | 3410 | Waterford Utd vs Longford Town | 2.03 | 3.44 | 3.20 |
| 21:45 | 3933 | Raith Rovers vs Dunfermline | 1.95 | 3.52 | 3.47 |
| 21:45 | 5999 | Shelbourne vs Bray Wanderers | 2.06 | 3.35 | 3.21 |
| 22:00 | 1260 | Al Ahly Cairo vs Al Masry Club | 1.39 | 4.15 | 8.69 |
| 22:00 | 1747 | Metalac vs FK Vozdovac | 1.79 | 3.38 | 4.16 |
| 22:00 | 2780 | Finn Harps vs St Patricks | 4.05 | 3.47 | 1.78 |
| 22:00 | 3963 | Betis vs Cadiz CF | 1.57 | 3.97 | 6.03 |
| 22:00 | 5496 | Brest vs Paris St Germain | 9.01 | 5.77 | 1.28 |
| 23:00 | 4057 | Almeria vs Real Oviedo | 1.80 | 3.31 | 4.64 |
| 23:15 | 2258 | Moreirense vs Sporting Braga | 5.12 | 3.54 | 1.67 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MADRID HAIJAKATA TAMAA KWA MBAPPE




**MADRID, Hispania**

REAL Madrid haijakata tamaa ya kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la Diario AS la jana Alhamisi.

Majaliwa ya Mbappe yameendelea kutawala mjadala kwenye vyombo vingi vya habari Ulaya.

Mkataba wa sasa wa Mbappe na Paris Saint-Germain unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22 na hajaonyesha nia ya kutaka kuongeza tena na miamba hao wa soka la Ufaransa.

Real Madrid imeripotiwa kuendelea kuwa na matumaini ya kuipata huduma ya nyota huyo mshindi wa Kombe la Dunia kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa kipindi hiki.

Mbappe yupo kwenye mwaka wake wa mwisho na PSG na Madrid wamekuwa wakipambana sana kuhakikisha wanamtoa nyota huyo katika jiji la Paris.

Ujio wa Lionel Messi kutoka Barcelona kipindi hiki, unatoa mwanya kwa Mbappe kuondoka hapo PSG, ingawa bado Madrid hawajapenyeza ofa yao.

Mbappe mwenyewe ameonyesha nia kubwa ya kutaka kuondoka na kwenda kujiunga na timu hiyo ambayo amekuwa akiota kuichezea kwa muda mrefu.

Hata hivyo, uongozi wa PSG ulishaweka wazi kwamba, mchezaji huyo hauzwi kwa kipindi hiki cha majira ya joto.

# Griezmann afurahia kufikisha mechi 100




**BARCELONA, Hispania**

ANTOINE Griezmann ana "furaha na ufahari" baada ya kufikisha mechi 100 alizoichezea Barcelona na Mfaransa huyo anawania kuweka historia ya miamba hao wa LaLiga.

Griezmann alifikisha idadi hiyo ya mechi Jumapili wakati Barcelona ikishinda mabao 4-2 dhidi ya Real Sociedad na amefunga jumla ya mabao 35.

Huku akiwa na changamoto ya kuibeba timu hiyo baada ya kuondoka kwa Lionel Messi aliyetua Paris Saint-Germain, kocha wa Barca, Ronald Koeman atakuwa na matumaini kwamba, atatengeneza upatina mzuri na Memphis Depay katika safu ya ushambuliaji.

Griezmann, ambaye aliwasili hapo Atletico Madrid mwaka 2019, ameiambia tovuti ya klabu hiyo jana: "Nina furaha na najisikia fahari kufikia idadi hii ya mechi.

"Lilikuwa jambo muhimu sana kupata ushindi kwenye mchezo wetu wa kwanza ambao mashabiki walirudi tena uwanjani, ambao hawajatuona kwa muda mrefu.

"Ulikuwa mchezo mzuri na matumaini yetu tutapata ushindi mwingine dhidi ya Athletic Bilbao."

Tangu alipowasili hapo mwaka 2019, hakuna mchezaji mwingine kwa sasa aliyeichezea nchi nyingi zaidi Barca, huku Messi akicheza kwa dakika 8,003 na Marc-Andre ter Stegen dakika 8,040, huku Griezmann akicheza jumla ya dakika 7,497.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Griezmann yupo nyuma ya Messi kwa kuhusika na mabao mengi kwa kipindi hicho, akiwa amehusika moja kwa mabao 51 yakiwa ni 19 zaidi ya mfungaji wa tatu wa wakati wote wa klabu hiyo, Luis Suarez, ambaye alishinda taji lake la kwanza la Atletico msimu uliopita.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ODEGAARD RASMI MALI YA ARSENAL

●●● Ni baada ya Madrid kuridhia uhamisho wake huku Barca ikijipanga kumsajili...

**LONDON, ENGLAND**

ARSENAL wamefikia makubaliano na Real Madrid kwa ajili ya kumsajili kiungo mshambuliaji, Martin Odegaard.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, ambaye atajiunga kwa ada ya awali ya pauni milioni 30 pamoja na bonasi, alikuwa jijini London jana kufanyiwa vipimo vya afya.

Makubaliano ya maslahi binafsi hayawezi kuwa tatizo na Sky Sports News inaelewa kwamba, Odegaard amechapata chanjo na hivyo hatahitaji muda wa kukaa karantini.

Kama usajili wake utakamilika kabla ya leo Ijumaa, Odegaard atakuwa kwenye mchezo wa Arsenal dhidi ya Chelsea Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita akicheza kwa mkopo hapo kwa washikabunduki baada ya kushindwa kupata namba kwenye kikosi cha Real Madrid chini ya kocha Zinedine Zidane.

Alicheza mechi 20 kwenye mashindano yote, huku moja ya mabao yake mawili kwa miamba hao wa London Kaskazini akifunga kwenye ushindi dhidi wa Tottenham Hotspur Machi, mwaka huu.

Waati huo huo, Arsenal pia wamefikia makubaliano na Sheffield United kwa usajili wa golikipa, Aaron Ramsdale kwa ada ya pauni milioni 24.

Na ada hiyo inaweza kuongezeka kwa pauni milioni sita ikitegemeana na kama Ramsdale atakuwa chaguo la kwanza la muda mrefu kwa washikabunduki hao.

Ramsdale amekuwa akiwaniwa na Mikel Arteta kipindi hiki cha majira ya joto, akiwa amejiunga na Sheffield United akitokea Bournemouth mwaka 2020.

Barcelona pia inawania kumsajili Pierre-Emerick Aubameyang kutoka hapo Arsenal.

Miamba hao wa LaLiga wapo tayari kumtoa ofa kiungo wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho kama sehemu ya mabadilishano na Arsenal.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, alisaini mkataba mpya wa miaka mitatu na Arsenal mwaka jana na mkataba wake upo hadi mwaka 2024.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon aliukosa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Brentford Ijumaa iliyopita kutokana na kuwa majeruhi pamoja na Alexandre Lacazette.

Aubameyang, ambaye alijiunga na Arsenal kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 60 Januari 2018, alifunga mabao 15 kwa miamba hao wa London Kaskazini msimu uliopita, huku timu hiyo ikishindwa kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya kwa kipindi cha miaka 25.

## ZISIKUPITE

### KANE SAFARI IMEKARIBIA
MANCHESTER City inatayarisha dau la pauni milioni 150 kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, huku vyanzo vikisema kitita hicho huenda kikatosha kuishawishi Tottenham na mwenyekiti wake Daniel Levy kuanza mazungumzo. ***(Independent)***

### VLAHOVIC ATAKIWA CITY
IKIWA Manchester City itashindwa kumpata Harry Kane msimu huu, inasemekana mabingwa hao wa Ligi Kuu England, wanafikiria kumchukua mchezaji wa kimataifa wa Serbia, Dusan Vlahovic (21), kama mbadala wake. City imeripotiwa kujiunga na wengine wanaomsaka mshambuliaji huyo wa Fiorentina kwa dau la euro milioni 80. (***Firenze Viola***)

### LIVERPOOL YAPATA PIGO
LIVERPOOL imepata pigo katika mbio zake za kumsaka kiungo wa kati wa Lille, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 24, ambaye huenda akakosa mechi kwa wiki sita kwa sababu ya jeraha. ***(Mirror)***

### ARSENAL YAMWANIA ASENSIO
ARSENAL huenda iko tayari kwa makubaliano ya mabadilishano yatakayogharimu kiasi cha pauni milioni 34 kumpata mchezaji wa Real Madrid raia wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes)***

### MILENNKOVIC KITAELEWEKA
KLABU ya Tottenham Hotspur imeimarisha nia yake ya kumsaka mlinzi wa Fiorentina raia wa Serbia, Nikola Milenkovic baada ya West Ham kuamua kutomfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(The Times)***

### SALAH MAMBO SAFI
MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, huenda akakubali kusaini mkataba wa muda mrefu na Liverpool. ***(Times)***

### LONGSTAFF SOKONI
NEWCASTLE imeweka kiwango cha dau la pauni milioni 10 kwa ajili ya kumuuza kiungo wa kati Sean Longstaff. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, huko St James' Park unafikia ukomo wake msimu ujao na kocha wa Everton, Rafa Benitez inasemekana anafikiria kufanya mazungumzo ya kumpeleka Goodison Park. ***(Mail)***

### TRIPPIER HAUZWI
ARSENAL na Manchester United zimeombwa kusahau kuhusu suala la kumsajili beki wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30. ***(AS)***

### EVERTON YAMTAKA HOPPE
EVERTON huenda ikamsajili mshambuliaji wa Schalke, Matthew Hoppe kwa dau la chini ya pauni milioni saba. Toffees hao ni moja ya timu kadhaa zenye nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, kwa kitita cha pauni milioni nne na bado itachukuliwa kama makubaliano mazuri ya kibiashara. ***(Bild)***

### HALAAND ATAJWA LIVERPOOL
LIVERPOOL inaongoza katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. (Sport1 via Sport1 via ***Mirror)***

### WATFORD YAIGOMEA PALACE
DAU la Crystal Palace la pauni milioni tano kwa kiungo wa kati, Will Hughes mwenye umri wa miaka 26, limekataliwa na Watford. ***(Sun)***

# MAKOCHA WAFUNGUKA SABABU ZINAZOWAKWAMISHA WAZAWA

**Na Ally Mlanzi, Tudarco**

WAKATI dirisha la usajili likiwa linaendelea katika mataifa mbalimbali kuelekea msimu mpya, makocha na wadau wa soka nchini wamesema wachezaji Watanzania wanakosa timu za nje ya nchi kwa sababu hawapendi kujituma ukilinganisha na nyota wageni wanaocheza katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wachezaji wa Simba, Clatous Chama raia wa Zambia, Luis Miquissone kutoka Msumbiji na Mkongomani Tuisila Kisinda wametawala vyombo mbalimbali vya habari kuhusiana na mchakato wa uhamisho wao kuelekea Morocco na Misri.

Chama na Miqiussone wametakiwa nje ya nchi baada ya kuonyesha viwango vya juu katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati Kisinda yeye aliisaidia vyema Yanga kupata matokeo mazuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA msimu uliomalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana na Mecky Maxime wa Kituo cha Kulea Vipaji cha Cambiasso, anasema, wachezaji wa hapa nchini wamekuwa wahapati klabu za nje kutokana na kushindwa kuonyesha uwezo wa juu katika mechi mbalimbali wanazocheza.

Maxime alisema nyota wa Tanzania wamekuwa na tabia ya 'kuridhika' tofauti na wageni ambao wanafahamu thamani na umuhimu wa kazi wanayoifanya.

"Wachezaji wetu hawakidhi soko la kimataifa kwa sababu ya kutoonyesha juhudi binafsi, hawaonyeshi viwango vizuri, kila timu inahitaji kusajili wachezaji wazuri, hata hao waliouzwa walionyesha viwango vizuri," alisema Maxime.

Kocha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Kagera Sugar alisema bado wanayonafasi ya kujituma na hatimaye wanaweza kufungua milango kwa mawakala wanaotafuta vipaji. "Umefika wakati wanatakiwa kubadilika, wajitahidi na kupambana, ili kuonyesha viwango vya juu, tutapata wachezaji wengi wazuri na watakaouzika nje ya Tanzania," Maxime alisema.

Naye Kocha wa Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 wa Kituo cha JKM Park, Noah Kanyage alisema wachezaji wengi wazawa hawajitumi wanapokuwa katika mazoezi na matokeo yake hucheza kwa kiwango cha chini kwenye mechi mbalimbali wanazopangwa.

"Tuna wachezaji wengi wenye vipaji vikubwa ila hawajitumi wanapokuwa mazoezini, utakuta mchezaji ana kipaji lakini hana jitihada, hili ni tatizo mojawapo," alisema Kanyage.

Kocha huyo aliongeza, wachezaji wengi wazawa wamekosa misingi mizuri ya mchezo huo pamoja na usimamizi wenye weledi, ukilinganisha na wenzao kutoka nje ya nchi.

Kiungo wa Yanga, Mukoko Tonombe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), naye anatajwa kuwindwa na timu za nje lakini klabu yake imekataa kumuuza nyota huyo.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Ukanda wa COSAFA yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 15, mwaka huu nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

## Polisi Tanzania yaibomoa Coastal

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Polisi Tanzania imezidi kujiimarisha kuelelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara kwa kumsajili winga wa Coastal Union ya jijini Tanga, Salim Kipemba.

Klabu hiyo imemtambulisha rasmi Kipemba kuwa ni mchezaji wake mpya ambaye atakuwa kwenye kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa mwaka 2021/22.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini alisema anajisikia furaha kuendelea na mchakato wa usajili ana anaahidi kuendelea na zoezi hilo kwa umakini.

Malale alisema anahitaji kuwa na kikosi imara na kitakachoonyesha ushindani kwenye mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA watakayochuana.

"Unajua usajili ni kama ndoa. Mtu unatakiwa ukosee vyote lakini siyo kuchagua mume au mke. Ni lazima umtafute na kumpata yule ambaye unaweza kuishi naye kwa kupendana na kuvumiliana, pia nidhamu. Hata wachezaji hivyo hivyo, unaweza kumpata mchezaji mzuri uwanjani, lakini nje ya uwanja ni matatizo matupu," alisema Malale.

Tayari Polisi Tanzania imeshawasajili wachezaji Vitalis Mayanga, Tariq Simba na Juma Makapu kutoka Yanga.

## Mwalimu Kashasha afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MCHAMBUZI na mtangazaji maarufu wa michezo nchini, Alex Kashasha, amefariki dunia jana akiwa katika hospitali ya Kairuki jijini Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu.

Kashasha ambaye alizaliwa mwaka 1957, alianza kupata umaarufu kutokana na maneno ya 'kisayansi' aliyokuwa akiyatumia wakati akitangaza mubashara mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, michezo ya Taifa Stars na mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi.



"Mchambuzi maarufu wa soka, Mwalimu Alex Kashasha, amefariki leo (jana), Agosti 19, 2021 alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Kairuki mkoani Dar es Salaam. Taarifa zaidi zitaendelea kutolewa," ilisema taarifa rasmi iliyotolewa na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC).

Kashasha alikuwa ni mtumishi wa TBC hadi umauti ulipomkuta hapo jana mchana.

## Hafidh, Vuai wapata ulaji ZFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limemteua Hafidh Ali Mohammed 'Shoka' kuwa Makamu wa Rais wa shirikisho hilo, imefahamika.

Katiba ya ZFF iliyofanyiwa marekebisho inampa mamlaka Rais wa shirikisho hilo aliyechaguliwa kuteua makamu wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa ZFF, Abdulatif Ali Yassin alisema uteuzi huo umefanyika kwa kufuatia matakwa ya katiba tofauti na zamani Makamu wa Rais alikuwa anapigiwa kura.

Yassin pia amemtangaza rasmi, Hussein Ahmada Vuai kuwa katibu Mkuu wa ZFF wakati Khamis Hamadi ameteuliwa kuwa Katibu Msaidizi huku Said Mohamed Abdulla yeye ameula katika nafasi ya Mkurugenzi wa Ufundi.

"Nina matumaini makubwa katika kufanya kazi kwa ushirikiano na watendaji wote wa ZFF ili tufikie malengo, lazima kwanza sisi wa ngazi za juu tuonyeshe mfano, kufanya kazi kwa umoja, na tusikubali kuingiza mambo ambayo hayataleta faida katika soka letu," alisema Abdulatif.

Kiongozi huyo alichaguliwa kuiongoza ZFF mapema mwaka huu, kwa ajili ya kuziba nafasi iliyoachwa na Kombo Pandu ambaye alitangaza kujiuzulu.

# Michezo

Ijumaa Agosti 20, 2021

Nipashe





## Odegaard rasmi mali ya Arsenal

**PASUA...**




Kocha Mkuu wa Timu Soka ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen, akizungumza kuhusiana na maandalizi ya mechi mbili za Kundi J za kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Madagascar zitakazochezwa mapema mwezi ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JEURI YA YANGA HII HAPA

## ●●● Inaanzia katika ubora wa magolikipa wake huku ikiweka wazi ITC za wachezaji...

**Adam Fungamwango na Tunu Hassan,**

**TUDARco**

WAKATI uongozi wa Yanga ukijivunia ubora wa magolikipa wake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari imepokea hati za uhamisho za wachezaji wake wa kimataifa isipokuwa kiungo, Mganda Khalid Aucho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wanaendelea na mchakato wa uhamisho wa Aucho ili aweze kuitumikia timu hiyo kuanzia mwanzoni mwa msimu huu.

Bumbuli alisema Yanga inajipanga kukamilisha taratibu zote muhimu zinazohitajika kwa wachezaji wake na waajiriwa wengine wa timu hiyo kama sheria za nchi zinavyoelekeza.

"Ni mchezaji mmoja tu ndiyo bado hajapata ITC, lakini wengine wote tayari tumekamilisha taratibu, kuhusu Mayele (Fiston), naye suala lake linafanyiwa kazi, tutatoa taarifa rasmi kwa sababu mpaka jana (juzi), Mkurugenzi wa Mashindano (Thabit Kandoro), alikuwa anakamilisha majadiliano ili kupata ITC ya Khalid Aucho," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema changamoto ya mawasiliano ya lugha ndio iliyokwamisha kumalizika mapema kwa uhamisho wa Aucho, lakini wanaamini atakuwa sehemu ya nyota watakaovaa jezi ya Yanga katika msimu ujao.

"Unajua wenzetu tunawaandikia kwa Kiingereza na wao mpaka iende sijui wapi ndio wajibu, mnapata barua ya kiarabu kwa hiyo ikawa shida kidogo, lakini hiyo sintofahamu imeshatatuliwa na jana (juzi) mchana kulikuwa na nyaraka zinatumwa katika klabu yake ili watoe barua ya ruhusa," alisema Bumbuli.

Kocha wa makipa wa Yanga, Razack Siwa aliliambia gazeti hili walinda mlango wapya waliosajiliwa katika timu hiyo, Djigui Diarra na Erick Johora wana vipaji vikubwa na ni silaha muhimu kuelekea msimu mpya.

Siwa alisema wachezaji hao wanajituma zaidi mazoezini na anaamini watakuwa msaada mkubwa kwa timu hiyo.

"Nimekaa nao muda mfupi, lakini nimegundua wana vipaji vikubwa na wanajituma, hiyo inanipa mimi ari ya kuzidi kuwafundisha mbinu mbalimbali ili kuwa bora zaidi," alisema raia huyo wa Kenya.

Kocha huyo alisema hataangalia rekodi za nyuma za wachezaji hao na atapendekeza kipa wa kuanza kutokana na kile atakachokiona kwenye mazoezi yanayoendelea.

"Mara nyingi kwenye mpira tunaangalia zaidi mchezaji anachokifanya sasa, siyo alichokifanya siku zilizopita. Kwa hiyo mimi nawaangalia, ni makipa wazuri wenye vipaji na kama wataendelea hivi na mazoezi, basi watazidi kuwa bora zaidi," Siwa alisema.

Diarra kutoka Mali na Johora ambaye ni Mtanzania aliyekuwa akicheza soka la kulipa nchini Burundi, wamesajiliwa Yanga kuziba nafasi zilizoachwa na Mkenya Farouk Shikalo na Metacha Mnata ambao walitemwa kutokana na kushuka kwa kiwango na makosa ya utovu wa nidhamu.

Wakati huo huo, Bumbuli alisema maandalizi kuelekea uzinduzi wa Tamasha la Wiki ya Mwananchi litakaloanzia Zanzibar Agosti 22, mwaka huu na kilele chake kitafanyika Dar es Salaam Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa yanaendelea vyema.

"Tutalifanya hili rasmi mjini Zanzibar, lakini hii itakuwa nchi nzima, kwa wanachama na mashabiki wetu popote walipo kufanya shughuli za kijamii kwenye maeneo yao ya karibu. Tunataka mwaka huu shamrashamra za Wiki ya Mwananchi ivunje rekodi ya ile ya mwaka jana. Na kwetu sisi kuna vitu ambavyo mwaka huu tumeviongeza ili kuleta burudani," alisema Bumbuli.

Kutoka Morocco, Meneja wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema mazoezi yanaenda vyema huku wachezaji na viongozi wote walioko huko wako fiti na wamefurahia kambi hiyo.

# Kabwili arejeshwa Taifa Stars

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen, ameita wachezaji 28 watakaojiandaa na mechi mbili za kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia akiwamo golikipa chaguo la tatu wa Yanga, Ramadhani Kabwili ambaye alikuwa nje ya kikosi hicho kwa muda mrefu.

Taifa Stars iliyoko Kundi J itakuwa mgeni wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Septemba 2, mwaka huu na baadaye itawakaribisha Madagascar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa siku tano baadaye.

Poulsen alisema kikosi hicho kitaingia kambini Jumanne na anatarajia kucheza mechi moja ya kirafiki ili kuwaimarisha wachezaji wake.

Aliwataja nyota watakaoingia kambini ni pamoja na Aishi Manula (Simba), Metacha Mnata, Kabwili (Yanga) na Wilbol Maseke (Azam FC), mabeki ni Shomari Kapombe, Israel Mwenda, Juma Kennedy, Mohammed Hussein (Simba), Dickson Job, Bakari Mwamnyeto (Yanga), Lusajo Mwaikenda na Abdulrazack Mohammed.

Wachezaji wengine ni Edward Manyama, Ayoub Lyanga (Azam FC), Meshack Mwaita (Gwambina FC), Nickson Kibabage (Youssufia FC - Morocco), Novatus Dismas (Muccabi Tel Avivi- Israel), Salum Abubakar, Iddy Nado na Mudathir Yahya (Azam FC), Feisal Salum, Zawadi Mauya (Yanga), Mzamiru Yassin, John Bocco (Simba), Abdul Selemani (Coastal Union) na Simon Msuva (Wydad).

"Muda ni mfupi, tunalazimika kujiandaa vizuri, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanapambana kutafuta timu kutoka nchi jirani ili kucheza mechi ya kirafiki, nina imani na wachezaji watafanya vizuri katika mechi hiyo na hata dhidi ya Madagascar tutakaocheza hapa nyumbani," alisema kocha huyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >